# GOLDLITE ONLINE SUPPLIES

## KCSE NATIONAL SCHOOLS TRIALS AND JOINT SERIES 2025

# KISWAHILI PAPER 3

KABARAK HIGH
ALLIANCE BOYS
ALLIANCE GIRLS
ASUMBI GIRLS
CRESCENDO JOINT
EAGLES JOINT
KISII SCHOOL
KENYA HIGH
LANJET JOINT
MANGU SCHOOL
MARANDA SCHOOL
MASENO SCHOOL
MERU SCHOOL
MIRROR JOINT
MOKASA JOINT 1
MOMALICHE
STAREHE GIRLS

**Compiled and distributed by Goldlite Online Supplies. For these and more inbox/text / WhatsApp 0724351706/0726960003. Marking schemes are available. Inbox now**

*These exams have been compiled from recently done national schools' trials and joint series*

# *KNEC COMPLIANT*

# GOLDLITE ONLINE SUPPLIES

*Cheti cha Kuhitimu Kisomo cha Sekondari*

## TATHMINI YA MAJARIBIO (I), 2025

**102/3 Kiswahili - Fasihi Karatasi ya 3**

**KIDATO CHA NNE 2025 Saa: 2½**

# SHULE YA UPILI YA MOI KABARAK

**Jina: ……………………………………Nambari: …………..Tarehe……................**

**Mkondo:………..............................Sahihi:……..................................................**

**<u>Maagizo</u>**

a) ***Andika jina lako, nambari ya usajili, mkondo, sahihi na tarehe katika nafasi ulizoachiwa hapo juu.***
b) ***Jibu maswali manne pekee.***
c) ***Swali la kwanza ni la lazima.***
d) ***Maswali hayo mengine matatu yachaguliwe kutoka sehemu nne zilizobaki; Riwaya, Hadithi Fupi, Ushairi na Fasihi simulizi***
e) ***Usijibu maswali mawili kutoka sehemu moja.***
f) ***Karatasi hii ina kurasa 18. Watahiniwa ni lazima wahakikishe kwamba kurasa zote za karatasi hii zimepigwa chapa sawasawa na kuwa maswali yote yamo.***

**Kwa matumizi ya mtahini pekee**

| SWALI | UPEO | ALAMA |
|---|---|---|
| 1 | 20 | |
| | 20 | |
| | 20 | |
| | 20 | |
| JUMLA | 80 | |

CONTACT US ON:
WhatsApp/Call or Text 0724351706/0726960003
EMAIL: Goldlitepublishers@gmail.com

## SEHEMU A: FASIHI SIMULIZI

1. **Lazima**

*Soma utungo ufuatao kisha ujibu maswali.*

(Akiuliza hadhira: Watu wetu mpo? Niimbe nisiimbe?)

Karembo Analia, Karembo Analia
Chozi lausaliti undani wake
Undani ambao ameuficha kwa miaka na mikaka
Undani ambao japo anachelea kutangaza asije akaonekana apendaye chongo…
Itabidi kuutoa, kuumwaga mtama

Na kiini cha chozi hili ni kwamba imewadia
Imewadia siku ya siku kanisani kwenda,
Kujitia pingu
Kujitia pingu, pingu za aushi
Je, hakuyataka haya?
Hakupania yapakata kama mwanagenzi,
Apakatavyo malaika mikonono pake?
Kwani basi analovya, kidari kwa maji chumvi?
Shavu lake laini, kuwa kijivu kwa shaka?
Ama ni yano mapenzi yalomlemea? Mapenzi
Alopania kwa miaka na dahari?

Kipi kinokwinamisha? Kwa
tewengu kukubwaga?
Ama ni majukumu kuhofia mwenzetu?
Ni adha za ulezi?
Ni hofu ya kutelekezwa
Jikoni kuachwa jukumu la kawaida?
Ama ni ugeni wa nasaba uso asili unokuuguza?
Je, ni mazoea unochelea kuacha?

CONTACT US ON:
WhatsApp/Call or Text 0724351706/0726960003
EMAIL: Goldlitepublishers@gmail.com

Ama uzito wa nanga ua huba?
Kipi, sema ewe mwenzangu, sema

Nikahi ni sitara
Usumbufu kuepuka vipanga na mwewe
Ndoa huneemesha na jina kukupa utatukuka kimwana
Shujaa ukapata wa kukulinda
Miliki ni hakikisho kutoka kwa dume hata katika mauko,
Penzi halali kupata, na warithi kuambulia,
Wa kiume kukufa
Silie mwana silie
Watutia simanzi
Waitia ndoa doa, nuksani kukuandamia.

Wavyele mpeni Baraka
Mashangazi mtemeeni mate
Viganja kumiminia pumzi zenu za neema
Ndoa yake kutengenea
Maumbu achene Kulengwa
Na machozi
Mwamlza zaidi, unyonge kumtia

Baba mtu shika kondooyo,
Mwongoze kidesturi, madhabahu karibia, Mkabidhi
mkweo, mwenzi wake wa maisha.
Ndiye takayechukua fahali, samba atakuwa akikaidi
Amri atatoa yeye, malkia kufuata,
Masase wake……………………
Yeye hutamka

CONTACT US ON:
WhatsApp/Call or Text 0724351706/0726960003
EMAIL: Goldlitepublishers@gmail.com

(a) Changanua utungo huu kimtindo. (alama 4)

(b) Kwa kutumia mifano **minne** mwafaka, eleza jinsi suala la taasubi ya kiume lilivyoangaziwa katika utungo huu. (alama 4)

(c) Eleleza manufaa **mawili** ya ndoa kulingana na wimbo huu. (alama 2)

(d) Unapanga kufanya utafiti kuhusu wimbo huu, fafanua changamoto ambazo huenda ukakumbana nazo. (alama 3)

(e) (Akiuliza hadhira: Watu wetu mpo? Niimbe nisiimbe?)" Eleza majukumu **matatu** ya kauli hii. (alama 3)

(f) Pendekeza mikakati **minne** ambayo serikali inafaa kuchukua ili kuzuia kupotea kwa wimbo huu katika jamii. (alama 4)

## SEHEMU B: RIWAYA

**Prof. Clara Momanyi:** *Nguu za Jadi*

*Jibu swali la 2 au 3.*

2."Unalichukia lile umbo lake la miraba minne?"

"Siwezi kulichukia maumbile ya Mwenyezi Mungu"

(a) Fafanua muktadha wa dondoo hili. (alama 4)

(b) Tambua mbinu **tatu** za kimtindo zinazojitokeza katika dondoo (alama 2)

(c) Eleza sifa **hasi nne** za msemaji wa kauli ya pili. (alama 4)

(d) Jadili umuhimu wa mrejelewa wa dondoo hili. (alama 4)

(e) Eleza sababu zinazomfanya mrejelewa kuchukiwa ukirejelea riwaya nzima. (alama 6)

3. (a) Changamoto zinazokumba wanajamii wa riwaya ya *Nguu za Jadi* ni sawa na zile zinazokumba mataifa ya Kiafrika. Thibitisha kwa hoja **kumi.** (alama 10)

(b) Eleza jinsi mwandishi alivyoshughulikia suala la ungozi mbaya katika riwaya hii. (alama 10)

## SEHEMU C: TAMTHILIA

**T. Arege:** *Bembea ya Maisha*

*Jibu swali la 4 au 5*

4. "Ulinipata mahututi kweli…Ilikua ajali mbaya. Zilipotea roho nyingi. Manusura tulikuwa watano tu. Bila msaada wako wa kuita Flying Doctors, hii leo ningekuwa nimesalia kwenye kumbukumbu tu. Mwezi mzima nilikuwa sijifahamu hospitalini. Japo hukunijua uliguswa ukaipigania nafasi yangu ya kuishi. Sijasahau. Daima nitashukuru kwa wema huu usio wa kawaida… Haikuwa rahisi. Niliponea tundu la sindano…"

CONTACT US ON:
WhatsApp/Call or Text 0724351706/0726960003
EMAIL: Goldlitepublishers@gmail.com

(a) Weka dondoo hili katika muktadha wake. (alama 4)

(b) Tambua toni ya dondoo hili. (alama 2)

(c) Fafanua mbinu **mbili** za kimtindo zilizojitokeza katika dondoo hili. (alama 2)

(d) Eleza umuhimu wa muktadha wa dondoo hili (alama 4)

(e) Jadili sifa **nne** za mrejelewa. (alama 4)

(f) Eleza maudhui yanayopatikana katika dondoo hili. (alama 4)

5. (a) Mwanamke wa Kiafrika ameonewa na jamii yake.Thibitisha kauli hii ukirejelea tamthilia hii. (alama 10)

(b) Maisha ya mwanadamu yamejaa kinaya. Eleza kauli hii kwa mujibu wa tamthilia ya Bembea. (alama 10)

## SEHEMU D: USHAIRI

*Jibu swali la 6 au 7*

6. *Soma shairi hili kisha ujibu maswali yafuatayo*

Bahati mbaya kuzawa, kwao hawa maskini
Hata kama nia kipawa, huwezi kukipateni
Taka sawa makiwa, na huende kuleleni
Nakataa kata kata, mie si bibi ni yaya

Asubuhi kuamka, nyumba ino naiosha
Moto pia naukoka, na watoto nawaosha
Chai pia naipika, hiyo kazi bade kwisha
Nakataa kata kata, mie si bibi ni yaya

Nimekaa sawa mama, nimelea siku nzima
Afikapo huyo mama, ni maswali chungu nzima
Najaribu kulalama, ananiiteni kima
Nakataa kata kata, mie si bibi ni yaya

CONTACT US ON:
WhatsApp/Call or Text 0724351706/0726960003
EMAIL: Goldlitepublishers@gmail.com

Mchana inapofika, Bwana nyumba huingia
Nami nafanya haraka, chakula namletea
Kula anakula haraka, kisha huanza nambia
Nakataa kata kata, mie si bibi ni yaya

Hamisha vyombo haraka, nina mengi ya kukupa"
Natoa vyombo haraka, kwa kweli ninamwogopa
Macho amenipachika, maji ninashindwa kumpa
Nakataa kata kata, mie si bibi ni yaya

(a) Tambua kichwa mwafaka cha shairi hili. (alama 1)

(b) "Mie si bibi ni yaya." Thibitisha ukweli wa kauli hii kwa hoja **nne.** (alama 4)

(c) Eleza bahari ya shairi hili kwa kuzingatia: (alama 3)

(i) Mishororo

(ii) Vina

(iii) Vipande

(d) Jadili maudhui moja **kuu** yanayojitokeza katika shairi hili. (alama 2)

(e) Eleza mbinu **nne** za lugha ambazo malenga wa shairi hili alitumia. (alama 4)

(f) Tambua toni ya shairi hili (alama 2)

(g) Andika ubeti wa pili kwa lugha tutumbi. (alama 4)

7. *Soma shairi hili kisha ujibu maswali yafuatayo*

Mimi ni kiumbe au upepo?
Mimi ni maji au mchanga
Nilidhani kuwa mimi ni kama wewe na wale
Kwa nii niadhibiwe hivi?

Uhai nilijua baada nukta chache
Na haya yote ni mapenzi ya Manani
Ewe mama, ewe baba mbona waniangamiza?
Kweli wasemavyo mkuki, kwa nguruwe

CONTACT US ON:
WhatsApp/Call or Text 0724351706/0726960003
EMAIL: Goldlitepublishers@gmail.com

Kilio,uchungu, machozi yapotelea gizani
Kwa nini hunisikii ee mvyele wangu?

Miezi majuma na siku ninataabika
Vilio uuu! Chooni, vilio uuu! majaani
Wana wa Mungu, mbona hunisikii?
Barabarani, mitoni ninaumwa na kudonwa na mbwa na ndege
Yaanii ulimwengu ni wa akina nani?
Niambie mama, niambie baba uuu

Siku ya kiyama imefika, hakika nitakuwepo
Baragumu itakapolia, mwenye kosa ajulikane
Mchezo mchafu mliofanya, mfurahie kunitupa
Kwa jicho pevu namwona, asali chungu mwailamba
Damu, mwili na mawazo yangu, pipani ninaoezeana
Mpenda raha, huhisi masaibu yangu?

Biblia, kurani na vitabu vingine, huonya
Kuua ni hatia, hakika si hatua
Kuua si kwa bunduki, panga au moto n.k
Vidonge, sindano, mitambo watumia,
Kuangamiza viumbe hafifu
Nimefahamu mwenye nguvu, ni wewe mama, baba
Ninaonya kizimbani, kwa Mungu tukutane
Oh! uchungu huu wa nini

(a) Thibitisha kuwa shairi hili ni shairi huru (alama 4)

(b) Eleza muundo wa ubeti wa mwisho. (alama 4)

CONTACT US ON:
WhatsApp/Call or Text 0724351706/0726960003
EMAIL: Goldlitepublishers@gmail.com

(c) Fafanua mbinu **tatu** ambazo zimetumika kutosheleza mahitaji ya kiarudhi. (alama 3)

(d) Tambua nafsineni katika shairi hili. (alama 2)

(e) Tambua njia nyingine **tatu** za kuua mbali na matumizi ya bunduki, panga na moto kwa mujibu wa shairi. (alama 3)

(f) Toa mfano wa mistari ifuatayo (alama 2)

(i) Mstari kifu

(ii) Mstari mshata

(g) Taja toni ya shairi hili. (alama 2)

## SEHEMU E: HADITHI FUPI

**D.W Letomia na Phibbian Muthama**: *Mapambazuko ya Machwo na Hadithi Nyingine.*

8. **D. W. Lutomia:** *Msiba wa Kujitakia*

Ahaaa! Mgeni aliyesubiriwa kwa hamu kuu mwishowe aliwasili. Msafara mkubwa wa walinzi wake uliambatana naye. Ulinzi mkali ambao ungemzuia hata nzi kupita karibu naye! Ndivyo walivyo waheshimiwa. Wakati wakiomba kura watatangamana na kusalimiana na kila mtu. Wakishapata walichokitaka wanajitenga na umma kama wagonjwa wa Ukoma!...alipigwa na butwaa! Hakuamini aliyoyaona. Ukumbini viti vinamkodolea macho. Sauti za wananchi zilisikika kwa umbali

(a) Fafanua muktadha wa dondoo hili. (alama 4)

(b) Changanua dondoo hili kimtindo. (alama 5)

(c) Jadili umuhimu wa muktadha wa dondoo hili (alama 5)

(d) Eleza jinsi mwandishi alivyoshughulikia suala la usaliti katika hadithi yake. (alama 6)

CONTACT US ON:
WhatsApp/Call or Text 0724351706/0726960003
EMAIL: Goldlitepublishers@gmail.com

# GOLDLITE ONLINE SUPPLIES

*Hati ya kuhitimu kisomo cha sekondari kenya(kcse*)

# MITIHANI YA PAMOJA YA SHULE ZA KITAIFA 2025
# STAREHE GIRLS' CENTRE MOCK EXAMINATION

**JINA: ……………………………………NAMBARI YA USAJILI: ………………………….**

**SAHIHI YA MTAHINIWA: ………………TAREHE: ………………DARASA: …...........**

**KISWAHILI KIDATO CHA NNE**

**KARATASI YA TATU**

**MUDAL SAA 2½**

**Maagizo**

**a)** *Andika jina lako, nambari ya usajili, mkondo, sahihi na tarehe katika nafasi ulizoachiwa hapo juu.*

***b)*** *Jibu maswali manne pekee.*

***c)*** *Swali la kwanza ni la lazima.*

***d)*** *Maswali hayo mengine matatu yachaguliwe kutoka sehemu nne zilizobaki Riwaya, Ushairi, Tamthilia na Fasihi Simulizi.*

***e)*** *Usijibu maswali mawili kutoka sehemu moja.*

***f)*** *Karatasi hii ina kurasa 6. Watahiniwa ni lazima wahakikishe kwamba kurasa zote za karatasi hii zimepigwa chapa sawasawa na kuwa maswali yote yamo.*

***g)*** *Maswali yote ni sharti yaandikwe kwa lugha ya Kiswahili.*

**Kwa matumizi ya mtahini pekee**

| SWALI | UPEO | ALAMA |
|---|---|---|
| 1 | 20 | |
| | 20 | |
| | 20 | |
| | 20 | |
| JUMLA | 80 | |

**CONTACT US ON:**

WhatsApp/Call or Text 0724351706/0726960003

EMAIL: Goldlitepublishers@gmail.com

## SEHEMU A: FASIHI SIMULIZI

1. a) Kwa kutumia vipengele vitano, onyesha maingiliano yaliyopo baina ya fasihi simulizi. (alama 5)

   b) Ni mambo gani huchangia kubadilika kwa kazi za fasihi simulizi? (alama 10

   c) Zitaje changamoto zozote tano za miviga katika jamii yoyote ile. (alama 5)

## SEHEMU YA B: RIWAYA NGUU ZA JADI:
## JIBU SWALI LA 3 AU 4

***2.*** „„,***Mrima, dunia yote inajua aliyemsaliti Yesu Kristo. Unajua mtu huyo aliishia wapi?***

a) Fafanua muktadha wa dondoo hili. (alama 4)

b) Tambua mbinu mbili za kimtindo zinazojitokeza katika dondoo hili. (alama 4)

c) Fafanua namna wahusika walivyowaendea kinyume wenzao katika riwaya ya Nguu za Jadi. (alama 12)

3. Bainisha nguu mbalimbali zilizotinga maendeleo ya nchi ya Matuo kulingana na riwaya ya Nguu za Jadi. (alama 20

## SEHEMU C: TAMTHILIA
## BEMBEA YA MAISHA (Timothy M.Arege)

***4.*** „„,***Walishasema baada ya dhiki ni faraja, Faraja ni zao la dhiki. Leo hii kikapu cha mama kimejaa ndago."***

a) Eleza **muktadha** wa dondoo hili. (alama 4)

b) Eleza vipengele **viwili** vya kimtindo kwenye dondoo. (alama 4)

c) Eleza maudhui **mawili** yanayodokezwa kwenye dondoo. (alama 2)

d) Eleza **sifa** za msemaji. (alama 5)

e) Kwa kutolea mifano mwafaka eleza dhiki alizopitia mama ambaye sasa kikapu chake kimejaa ndago. (alama 5)

5. Ukilazwa tayari unakuwa umeonja seli.Hata wahudumu wenyewe hawana mlahaka mwema .amri na vitisho kama askari.Unashindwa kama uuguze moyo ama ugonjwa.Katika wodi hewa iliyojaaa harufu ya dawa imezagaa,vitanda vimesalimu amri mpaka shiti zikagura.Yaani hali nzima haikupi matumaini ya kutoka ukiwa bora.matumaini yanadidimia .Tumaini lako unaliweka katika sala.

(a) Tambua toni mbili katika kifungu hiki (alama 2)

(b) Tambua aina moja ya taswira katika dondoo hili (alama 2)

(c) Kando na taswira chambua vipengele vingine vya kimtindo (alama 6)

(d) Fafanua namna mandhari ya dondoo hili yalivyochangia kujenga tamthilia ya bembea ya maisha (alama 10)

**CONTACT US ON:**
WhatsApp/Call or Text 0724351706/0726960003
EMAIL: Goldlitepublishers@gmail.com

## SEHEMU D: HADITHI FUPI

**6. Winnie Nyaruri Ogenche; Sabina**

"***Ninaomba wazazi wenzangu muwape watoto wa kike elimu badala ya kuwaoza mapema. Hongera, mwanangu kwa kupata alama mia nne arubaini na saba"***

a) Eleza umuhimu wa mrejelewa katika kukuza hadithi husika (alama5)

b) Tambua mbinu ya kimtindo iliyotumika katika dondoo hili (alama1)

c) Fafanua jinsi mbinu yenyewe ilivyotumika ili kufanikisha utunzi wa hadithi (alama6)

d) Fafanua changamoto zinazokabili jinsia ya kike kwa mujibu wa hadithi (alama8)

7. a) Jadili umuhimu wa barua ya mkewe suluhu katika kuijenga hadithi ya Kifo N cha Suluhu. (alama 10)

b) Fafanua swala la ajira kama linavyojitokeza katika hadithi, Harubu ya maisha. (alama 10)

**8. SEHEMU YA E : USHAIRI**

***Soma shairi lifuatalo kisha ujibu maswali.***

**ADA YA MJA**

Ada ya mja, ikimnyea mvua, hulalama ,kuzilaani mbingu
Ada ya mja, ikimchoma jua, hunung"una, kutukana majira.

Ada ya mja, apatapo mali, hazimtoshi, atafyonza zaidi Ada ya mja, apatapo cheo, hakimtoshi atapiggania ukubwa.

Ada ya mja, apatapo mke, ataongeza, hajalishwi na urembo. Ada ya mja, apatapo mume, atamshuku, udini haumshtui

Ada ya mja, zimpandapo hamaki, hutenda, nakujutia nadae Ada ya mja zimpatapo furaha, huhidi, na kushindwa kulipa.

Ada ya mja, kucheka kovu asiyekuwa, asiyekuwa nanajeraha Ada ya mja, kucheka kilema, ashindwapo, hali kwao kipo.

Ada ya mja, aonapo neno, husema neno, na kupatwa na neno. Ada ya mja, kula kutamu, kulima mavune, kwamshinda.

**Maswali**

a) Hili ni shairi la aina gani? Eleza. (alama 2)

b) Bainisha nafsi neni katika shairi hili (alama 2)

c) Fafanua hulka zozote nne za mja (alama 4)

d) Eleza muundo wa shairi hili (alama 4

**CONTACT US ON:**
WhatsApp/Call or Text 0724351706/0726960003
EMAIL: Goldlitepublishers@gmail.com

e) Tambua aina mbili za urudiaji zilizotumiwa katika shairi hili. (alama 2)

f) Andika ubeti wa tatu katika lugha nathari (alama 2)

g) Eleza toni ya shairi hili (alama 2)

h) Tambua mifano miwili ya methali zilizodokezwa kwenye shairi hili (alama 2)

**CONTACT US ON:**
WhatsApp/Call or Text 0724351706/0726960003
EMAIL: Goldlitepublishers@gmail.com

# GOLDLITE ONLINE SUPPLIES

***Hati ya kuhitimu kisomo cha sekondari kenya(kcse)***

# MITIHANI YA PAMOJA YA SHULE ZA KITAIFA 2025

JINA………………………………………………………………………….NAMBARI………….

**102/3**

**Kiswahili – Fasihi**

**Karatasi ya 3**

**Muda: Saa 2 $^1/_2$**

## SHULE YA UPILI YA WAVULANA YA ALLIANCE

**Maagizo**

***a)*** *Jibu maswali manne pekee. (b)*
*Swali la kwanza ni la lazima.*

***b)*** *Maswali hayo mengine matatu yachaguliwe kutoka sehemu nne zilizobaki yaani:Ushairi,Hadithi Fupi, Tamthilia na Riwaya.*

***c)*** *Usijibu maswali mawili kutoka sehemu moja.*

***d)*** *Andika nambari ya maswali uliyoyajibu kwenye jedwali ulilochorewa hapo chini.*

**Kwa matumizi ya mtahini pekee**

| Swali | Upeo | Alama |
|---|---|---|
| 1. | 20 | |
| | 20 | |
| | 20 | |
| | 20 | |
| Jumla | 80 | |

## SWALI LA LAZIMA.

## SEHEMU YA A: FASIHI SIMULIZI

1. **Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali yafuatayo;**

i) Kufa kupona.

a) Tambua utanzu na kipera cha utungo ulichopewa. **(alama 2)**

b) Tambua kipengele kimoja cha kimtindo katika utungo huo. **(alama 1)**

c) Taja vigezo vyovyote vinne vya kuainisha utungo wa namna hii. **(alama 4)** d) Eleza dhima tatu za utungo huu katika jamii. **(alama 3)**

ii) Kakangu analilia mwituni. – Shoka

a) Eleza muundo wa utungo huu. **(alama 2)**

b) Eleza sifa nne za utungo huu. **(alama 4)**

c) Unanuia kukusanya data nyanjani kuhusu kipera hiki. Eleza changamoto zitakazokukabili wakati wa shughuli hii. **(alama 4)**

## SEHEMU YA B: HADITHI FUPI

Timothy M. Arege.: ***Bembea ya Maisha***

**Jibu swali la 2 au la 3**

2. **Soma dondoo lifuatalo kisha ujibu maswali yafuatayo:**

"Unayafanya makubwa bure mwenzangu. Unafahamu vizuri kuwa hiyo si hulka yangu. Sasa mimi nina haja gani kuuvunja mji?"

(a) Eleza muktadha wa dondoo hili. **(alama4)**

(b) Bainisha toni ya msemaji. **(alama2)**

(c) Msemaji amepitia dhiki mbalimbali katika jamii yake, Tambua dhiki alizopitia. **(alama4)**

(d) Onyesha namna maudhui ya mgogoro yanavyojitokeza katika tamthilia nzima**(ala10)**

**AU**

3. *"Sasa kichwa hicho kisizunguke? Kikae pale pale ndiyo ujue ni kichwa? Kichwa kazi yake kuzunguka. Lipi lisilozungusha kichwa? Kutafuta lisilokizungusha kichwa ni kama kuwinda hewa kutaka kufumbata kwenye konzi."*

a) Changanua mtindo katika dondoo hili. **(alama 3)**

b) Eleza umuhimu wa msemaji wa maneno haya katika kukuza tamthilia ya Bembea ya Maisha..**(alama 5)**

**c)** Asasi ya ndoa inakumbwa na changamoto nyingi katika maisha. Thibitisha kwa kurejelea tamthilia ya Bembea ya Maisha. **(alama 12)**

## SEHEMU YA C: HADITHI FUPI

D.W Lutomia na Phibbian Muthama: *Mapambazuko ya Machweo na Hadithi Nyingine*

**Jibu swali la 4 au la 5**

**4.** "Enhee! Mpaka sasa hukupata nafasi ya kupiga simu, au angalau kutuma arafa?" "Samahani ... ulipopiga nilikuwa barabarani, singeweza kupokea simu."

(a) Eleza muktadha wa dondoo hili. **(alama 5)**

(b) Tambua toni katika dondoo hili. **(alama 1)**

(c) Eleza vipengele viwili vya kimtindo katika dondoo hili. **(alama 2)**

(d) Eleza sifa nne za aliyekuwa barabarani akapigiwa simu na kushindwa kuipokea.
( **(alama 4)**

(e) Harubu ni sehemu ya maisha ya binadamu. Hakiki kauli hii kwa hoja nane kwa kurejelea hadithi Harubu ya Maisha. **(alama 8)**

**AU**

**5.** *…akikiomba radhi kile kitawi cha mti kilichonasa kwenye kazu yake ya rangi ya udongo iliyoficha kiwingu cha nongo kwa kukosa kuoshwa tangu ainunue! Nikauacha mpambano ule kati ya mzimu na mwenye dhamana ya mzimu ambao sina shaka ulidumu hadi asubuhi pale wanakijiji walipofika kushuhudia siri nzito iliyomezwa na mzimu ule waliokuwa wakiogopa na kuamini kiasi cha kuabudu kwa unyenyekevu na uchaji uliotukuka!*

**(a)** Eleza muktadha wa dondoo. **(alama 4**

(b) Fafanua umuhimu wa mandhari katika dondoo hili. **(alama 4)**

(c) Fafanua mbinu za kimtindo katika dondoo. **(alama 4)**

(d) Onyesha jinsi itikadi ilivyomwezesha 'mwenye dhamana ya mizimu' na wenzake kuwafanya wanakijiji kuogopa na kuamini Mzimu wa Kipwerere kiasi cha kuabudu kwa unyenyekevu na uchaji uliotukuka. **(alama 8)**

## SEHEMU YA D: HADITHI FUPI

C. MOMANYI: **Nguu Za Jadi**

**Jibu swali la 6 au la 7**

**6.** "Lazima amejiunga na kundi la marafiki wenye pesa wanaojaribu kumpotosha."

(a) Eleza muktadha wa dondoo. **(alama 4)**

(b) Anayesema maneno haya ni jasiri. Thibitisha kwa hoja tano. **(alama 5)**

(c) Tathmini kwa hoja kumi na moja nafasi ya wenye pesa katika kuendeleza tamaa na ubinafsi katika nchi ya Matuo.
**(alama 11)**

AU

**7.** *"Mangwasha siku zote hizi ulikuwa unachezeshwa kayamba tu. Ati walisema Osama alikuwa hatari kwa usalama duniani; kuna Osama kuliko huyu?" alijiskia kusema. Alishusha pumzi kwa nguvuakajiuliza kimoyomoyo kwa nini Mungu aliruhusu moto kumtia kwenye shimo la maangamizi na wanawe.Hata hivyo, aliamini kuwa wakati mwingine Mungu huruhusu mabaya kutokea ili kuwafunza waja. Waaidha, alijua kuwa mashaka yanapomkumba mja, huwa ni funzo pia. Humtayarisha kuyahimili machungu zaidi ulimwenguni ama kumuasa dhidi ya kuabudu maovu. Maovu yanapotendwa na wachache, hata wale wasio na hatia pia hujikuta wamo humo uovuni. Ni mtego wa waliomo na wasiokuwemo.*

a) Changanua mtindo katika dondoo hili. **(alama 5)**

b) Eleza umuhimu wa mandhari ya kanisani aliko Mangwasha katika kukuza Riwaya ya Nguu za Jadi **(alama 5)**

c) Nchi ya matuo imeshinikizwa na Nguu Za Jadi zinazorudisha nyuma usawa katika jamii. Tathmini kauli hii kwa hoja kumi. **(alama 10)**

## SEHEMU YA E: USHAIRI

**8. Soma shairi lifuatalo kisha uyajibu maswali**

Mungu naomba subira, subira nayo imani
Imani iliyo bora, bora hapa duniani
Duniani mwa kombora, kombora nayo hiani
Hiani pamwe ukora wenye kuhini.

Kuhini kwenye kiburi, kiburi na
ufidhuli Ufidhuli wa kudhuri, kudhuri
wangu muwili Muwili hata kidari,
kidari kuwa thakili Thakili kisinawiri,
kisinawiri misuli.

Misuli kuwa hafifu, hafifu kama
muwele Muwele wa hitilafu, hitilafi
ya nduwele Nduwele kutakilifu,
kutakilifu milele Milele kutoniafu,
kutoniafu na vishale.

Vishale vinitomele, vinitomele
vikwato Vikwato pia maole, maole
kufanya mito Mito ya matozi tele,

tele mithili kitoto Kitoto kilo vipele,
vipele vyenye fukuto.

Fukuto lanipa neno, neno hili
kutamka Kutamka wazi vino, vino
subira kutaka Kutaka imani mno,
mno n’sipate wahaka
Wahaka wa matukano, matukano na mashaka.
Mashaka haya ya leo, leo yawe yamepita
Yamepita na vilio, vilio vipishe nyota
Nyota njema ing’arao, ing’arao kunikita
Kunikita salamani, salamani nikadata.

**Maswali:**

**(a)** Kwa nini nafsi neni inaomba subira na imani? **(alama2)**

**(b)** Shairi hili ni la aina gani kwa kuzingatia **(alama4)**

   **(i)** Mpangilio wa maneno

   **(ii)** Mpangilio wa vina.

**(c)** Kwa kutolea mifano eleza mbinu mbili za lugha zilizotumika katika shairi. **(alama4)**

**(d)** Andika ubeti wa tatu kwa lugha nathari. **(alama4)**

**(e)** Kwa kutolea mifano, eleza jinsi uhuru wa kishairi ulivyotumiwa kutekeleza arudhi.
( **(alama6)**

# GOLDLITE ONLINE SUPPLIES

*Cheti cha Kuhitimu Kisomo cha Sekondari*

## TATHMINI YA MAJARIBIO (I), 2025

**102/3 Kiswahili - Fasihi Karatasi ya 3**

**Saa: 2½**

# SHULE YA UPILI YA WASICHANA YA ALLIANCE

**JINA………………………………………….…………. NAMBARI YA MTAHINIWA…..............…**

**SAHIHI……………………TAREHE……………………..DARASA………………………**

**<u>MAAGIZO:</u>**

a) *Andika jina lako na nambari yako ya usajili katika nafasi ulizoachiwa hapo juu*
b) *Tia sahihi kisha uandike tarehe*
c) *Jibu maswali **<u>manne</u>** pekee*
d) *Swali la kwanza ni la lazima*
e) *Maswali hayo mengine **matatu** yachaguliwe kutoka sehemu nne zilizobaki yaani Riwaya, Tamthilia,Ushairi na Hadithi Fupi*
f) *Usijibu maswali **<u>mawili</u>** kutoka sehemu moja*
g) *Majibu yote **<u>lazima</u>** yaandikwe kwa lugha ya Kiswahili*

**<u>KWA MATUMIZI YA MTAHINI PEKEE</u>**

| Swali | Upeo | Alama |
|---|---|---|
| 1 | 20 | |
| | 20 | |
| | 20 | |
| | 20 | |
| **Jumla** | **80** | |

*CONTACT US ON:*
*WhatsApp/Call or Text 0724351706/0726960003*
*EMAIL: Goldlitepublishers@gmail.com*

## SEHEMU A:

## FASIHI SIMULIZI

**1. LAZIMA**

**Soma kifungu hiki kisha ujibu maswali**

Lala mtoto lala*2
Mama atakuja lala
Alienda sokoni lala
Aje na ndizi lala
Na maziwa ya mtoto lala
Kukupa kwangu wewe kinofu
Kipenzi mwana lala*2

Lala mtoto lala*2
Basi kipenzi lala
Baba atakuja lala
Aje na mkate lala
Mkate wa mtoto lala
Tanona ja ndovu lala

**Maswali**

a) Huku ukithibitisha jibu lako eleza huu ni wimbo wa aina gani? (alama 2)
b) Eleza sifa za wimbo wa aina hii. (alama 5)
c) Onyesha umuhimu wa wimbo huu. (alama 4)
d) Eleza ni shughuli gani za kiuchumi ambazo jamii hii inajihusisha nayo katika wimbo huu. (alama2)
e) Tambua mbinu zozote mbili za lugha zilizotumika katika wimbo huu. (alama 2)
f) Fafanua changamoto **tano** ambazo mtafiti anaweza kumbana nazo akiwa nyanjani. (alama 5)

## SEHEMU YA B:

## RIWAYA- NGUU ZA JADI

**Jibu swali la 2 au 3**

2. Hivyo, alitaka kubadili hali hata kama ilimaanisha kukitia kichwa chake kinywani mwa simba. Alitaka kuliokoa jahazi lililokuwa likielekea mwambani kwa kasi. Lakini angeliweza vipi kupambana na utandu wa mahasidi hao?.

(a) Eleza mbinu nne za kimtindo zinazojitokeza katika dondoo hili (alama 4)

(b) Eleza sababu za msemaji kutaka kufaulisha kauli iloyopigiwa mstari (alama 10)

(c) Eleza umuhimu wa mrejelewa katika kuijenga riwaya hii (alama 6)

**au**

3. Dunia yote inajua aliyemsaliti Yesu Kristo. Unajua mtu huyo aliishia wapi?

a) Fafanua muktadha wa dondoo hili (alama 4)

b) Tambua mbinu mbili za kimtindo zinazojitokeza katika dondoo hili. (alama 4)

c) Fafanua namna wahusika walivyowaendea kinyume wenzao katika riwaya ya Nguu za Jadi. (alama 12)

## SEHEMU C: TAMTHILIA;

## BEMBEA YA MAISHA – TIMOTHY M. AREGE

**Jibu Swali la 4 au 5.**

4. **“Huku ndiko kuvumilia hasa. Tazama faraja ilivyoalika sasa”**

a) Weka dondoo hili katika muktadha. (alama 4)

b) Eleza sifa za msemaji katika dondoo. (alama 6)

c) Onyesha jinsi faraja ilivyoalika katika maisha ya msemewa kwa kurejelea tamthilia ya: Bembea ya Maisha. (alama 10)

**AU**

**5.(a) Changanua mtindo katika kifungu kifuatacho. (alama 10)**

Maskini mke wangu! Kumbe ugonjwa haukumsaza mwaka baada ya mwaka. Umemla bila huruma. Awali niliona kama mchezo. Kumbe ilikuwa kweli! Kauli yake ninaona imesimama. Ni

mwele hakika. Laiti ningejua, jana ningeishi tofauti. Silesi zetu za maisha tungezila zilivyokuja kwa furaha. (*Kimya*). Siku hazigandi wala jana hairudi. Sasa jana imebaki kuwa kumbukizi baada ya kusombwa na wakati mfano wa mafuriko msimu wa masika. (*Kimya*). Kwa bahati nzuri bado tupo. Ninaweza kuiachia dunia tabasamu iwe silesi kwa vizazi vijavyo na kila mwenye nia njema. (*Kimya*). Siwezi kuendelea kuishi hivi. Sasa nimekata shauri. Lazima niache njia ya zamani na kuifuata mpya. Maisha mapya. Pombe! *(kama anayeisemea pombe).* Umenichezesha kama mwanasesere kwa muda mrefu. Umeninyima fursa ya kuielewa familia yangu. Hapana! Siku zangu za uzeeni lazima nizitumie kumwangalia mke wangu mgonjwa. Lazima nimshukuru kwa vitendo kwa jinsi alivyojitolea kuijenga familia yetu. *(anapunga mkono.)* Kwaheri pombe. Buriani.

b) Bainisha toni ya dondoo hili. (alama 2)

c) Fafanua umuhimu wa msemaji wa maneno haya katika kuijenga tamthilia nzima. (alama 8)

## SEHEMU YA D

## USHAIRI

**Jibu swali la 6 au la 7.**

6. **Soma shairi lifuatalo kisha ujibu maswali:**

Binadamu hatosheki, ni kiumbe chenye zani, kweli mja hapendeki,
Kwa kweli haaminiki, hila ameficha ndani, la wazi ni unafiki
Ukweliwe haafiki, njama zake zi moyoni, usimwone ni rafiki
Mtu kuwa na tamaa, akitaka kiso chake, ni hatari kama nyoka.

Wengine watakuua, wakiona una pesa, hata zikiwa kidogo,
Hizo kwao ni maua, hupupiwa zikatesa, wakazifuata nyago,
Hadi kwenye wao ua, pasipo hata kupesa, wala kukupa kisogo,
Mtu kuwa na tamaa, akitaka kiso chake, ni hatari kama nyoka

Pindi kinunua kitu, hafurai Shaitani, bali tajawa chukizo,
Mtu kiwa mtukutu, tanunua mtimani, kwalo lako tekelezo,
Tamko lake 'Subutu', kuondoa tumaini, na kukuulia wazo,
Mtu kuwa na tamaa, akitaka kiso chake, ni hatari kama nyoka,

Aliye na taraghani, taabu kuishi naye, kazi yake kujidai,
Takusema faraghani, asosema kiwa naye, kupendeza maadui,
Hana faida nyumbani, ni mtu akuchimbaye, mradi usitumai,
Mtu kuwa na tamaa, akitaka kiso chake, ni hatari kama nyoka,

Kwa hakika ni balaa, kumkirimu mchawi, aliejaa uchoyo,
Bahati ina hadaa, kukupa alo sadawi, aibatili rohoyo
Mipangoyo kwake jaa, na nia ya ustawi, huwiza vunja kaniyo,
Mtu kuwa na tamaa, akitaka kiso chake, ni hatari kama nyoka

Ninacho change killo, ninalia sanasana, kinyesi nimetupiwa,
Ningetoa azimio, lakini uwezo sina, kwa matatizo kuambiwa,
Ama nitumie mbio, fuadi ninanena, akilini nazuiwa,
Mtu kuwa na tamaa, akitaka kiso chake, ni hatari kama nyoka.

**MASWALI:**

a) Lipe shairi hili anwani mwafaka. (alama 1)

b) Fafanua mambo **matatu** ambayo nafsineni analalamikia. (alama 3)

c) Ainisha shairi hili kwa kuzingatia vigezo vifuatavyo. (alama 3)

(i) Idadi ya vipande katika kila mshororo

(ii) Mpangilio wa vina katika kila ubeti

(iii) Idadi ya mishororo katika kila ubeti

d) Andika ubeti **wa nne** katika lugha nathari. (alama 4)

e) Bainisha tamathali mbili za usemi zilizotumiwa katika shairi hili. (alama 2)

f) Huku ukitoa mifano, onyesha mbinu mbili alizotumia mshairi kutosheleza mahitaji ya kiarudhi. (alama 2)

g) Andika aina mbili za urudiaji zilizotumiwa katika shairi hili. (alama 2)

h) Fafanua muundo wa ubeti **wa tano**. (alama 3)

AU

**7. Soma shairi lifuatalo kisha ujibu maswali.**

Na ujenge nyumba yako, jingi jasho likuoshe,

Ufyeke, upime na uweke nguzo,

Kisha paa uweke na ukandike,

Siku nyingi bila kuingiliwa na mgeni hutakaa.

Wataanza kutalii mpaka mende usiku,

Nje na ndani ya  nyumba watazunguka,

Bila woga, bila ruhusa ulichonacho watakula,

Masalia yatakuwa yako, ijara ya kaziyo.

Na nyingi dawa uweke, nyumba nzima uihame,

Ukae nje nzima siku usubiri,

Wazima wamelala ukirudi usiku,

Vichwa vigumu hawafi mende rahisi.

Kifo cha mende sharti miguu juu

Kichwa ukikanyage kipasuke usikie,

Na kisha wengine usiku mchana uwasake.

Mpaka watakapokwisha.  Usiseme nao.

**Maswali**

(i)  Hili ni shairi la aina gani? (alama 1)

(ii) Eleza **muundo** wa shairi hili (alama 3)

iii) Eleza jinsi mshairi alivyoutumia **uhuru** wake katika utunzi wa shairi hili. (alama 4)

iv)Taja mbinu **mbili za lugha** alizotumia mshairi na uzitolee mifano. (alama 4)

v)Andika **ubeti wa tatu** kwa lugha nathari. (alama 4)

vi)Eleza **ujumbe** wa mshairi. (alama 2)

vii)Toa mfano mmoja wa mshororo **mshata**. (alama 1)

viii)Kichwa gani kinaliafiki shairi hili? (alama 1)

**SEHEMU E:**

**HADITHI FUPI**

**Mapambazuko ya Machweo na Hadithi Nyingine.**

**8. Harubu ya maisha *Paul Nganga Mutua***

“Naja. Nakamilisha shughuli ndogo hapa kisha nianze safari…”

(a) Weka dondoo hili katika muktadha wake (alama 4)

(b) Eleza sifa sita za msemaji wa kauli hii (alama 6)

(c) Jadili changamoto wanazokumbana nazo waajiriwa kwa kurejelea hadithi hii. (alama10)

# GOLDLITE ONLINE SUPPLIES

*Hati Ya Kuhitimu Kisomo Cha Sekondari Kenya(Kcse)*

**MITIHANI YA PAMOJA YA SHULE ZA KITAIFA 2025**

**JINA: ……………………………NAMBARI YA USAJILI: ………………………….**

**SAHIHI YA MTAHINIWA: ……………………TAREHE: ……DARASA: …............**

# SHULE YA UPILI YA WASICHANA YA ASUMBI

***MAAGIZO:***

***a)*** *Andika jina lako na nambari yako ya mtihani katika nafasi ulizoachiwa hapo juu.*

***b)*** *Tia sahihi yako kisha uandike tarehe ya mtihani katika nafasi ulizoachiwa hapo juu.*

***c)*** *Jibu maswali **manne** pekee.*

***d)*** *Swali la **kwanza** ni la **lazima.***

***e)*** *Maswali hayo mengine matatu yachaguliwe kutoka sehemu nne zilizobaki; yaani; Riwaya, Tamthilia, Ushairi, Hadithi Fupi .*

***f)*** *Majibu yote **lazima** yaandikwe kwa lugha ya Kiswahili*

***g)*** *Karatasi hii ina kurasa **6** zilizopigwa chapwa*

***h)*** *Watahiniwa ni **lazima** wahakikishe kwamba kurasa zote za karatasi hii zimepigwa chapa sawasawa na kuwa maswali yote yamo.*

***KWA MATUMIZI YA MTAHINI PEKEE.***

| Swali | Upeo | Alama |
|---|---|---|
| 1 | 20 | |
| | 20 | |
| | 20 | |
| | 20 | |
| Jumla | 80 | |

**CONTACT US ON:**
**WhatsApp/Call or Text 0724351706/0726960003**
**EMAIL: Goldlitepublishers@gmail.com**

**SWALI LA I (LAZIMA):**
**TAMTHILIA: BEMBEA YA MAISHA**

1. "Asiyejua safari ya Sara na Yona akielezwa huiona kama filamu'

a) Eleza muktadha wa dondoo hili (alama 4)
b) Eleza vipengele viwili vya kimtindo katika dondoo hili (alama 2)
c) Eleza sifa za mrejelewa wa maneno haya (alama 4)
d) Fafanua umuhimu wa mazungumzo kati ya Yona, Luka na Beni katika kuijenga Tamthilia ya Bembea ya Maisha (alama 10)

**SEHEMU YA B: NGUU ZA JADI**
**JIBU SWALI la 2 au la 3**

**2.** Hakika kila mtu ni mhusika mkuu katika kisa cha maisha yake mwenyewe."

a. Fafanua muktadha wa dondoo hili. (alama 4)
b. Thibithisha ukweli kuwa mrejelewa wa maneno haya aliipa hadhira yake kitu cha kuwatia moyo. (alama 8)
c. Fafanua maudhui ubabedume katika riwaya hii. (alama 8)

**3.** Riwaya ya Nguu za Jadi inadhihirisha jamii iliyojaa uozo.Thibitisha ukweli wa kauli hii. (alama 20)

**SEHEMU YA C: USHAIRI**

**JIBU SWALI LA 4 AU 5**

**4. USHAIRI**

***Soma shairi lifuatalo kisha ujibu maswali.***

Binadamu ana kero, li ndani ya moyo wake,
Hupenda yalo mororo, yote yasadifu kwake,
Yanayoleta mataguro, hukwepa yasimfike,
Hiyo ni yake kasoro, kiumbe binaadamu.

Milele katu hakiri, kupokonywa kilo chake,
Lakini huwa tayari, kudhulumu vya mwenzake,
Na kujifanya hodari, kila lake liongoke,
Na hiyo yake kasoro, kiumbe binaadamu.

Kutwaa asichopewa, pia ni tabia yake,
Ubishi kabarikiwa , hivyo ni vilima vyake,
Kama hayo kitendewa, hakiri ikubalike,
Pia ni kasoro yake, kiumbe binaadamu.

Mwepesi wa kuchokoza, pia ni mtindo wake,
Ambae hajamuanza, humtafutia lake,

**CONTACT US ON:**
**WhatsApp/Call or Text 0724351706/0726960003**
**EMAIL: Goldlitepublishers@gmail.com**

Na puresha kumjaza, mradi akasirike,
Nayo ni kasoro yake, kiumbe binaadamu.

Hakika binaadamu, kwa ule uzito wake,
Kawekewa jahanamu, likawe ni pigo lake,
Hiyo siku ya hukumu, adhabu zikamfike,
Kwa zile kasoro zake, kiumbe binaadamu.

(a) Kwa hoja **sita**, fafanua mtazamo wa mtunzi wa shairi hili kuhusu binadamu. (alama 6)
(b) Eleza muundo wa shairi hili. (alama 4)
(c) Bainisha vipengele **vitatu** vya kimtindo katika shairi hili. (alama 3)
(d) Fafanua aina **tatu** za uhuru wa kishairi katika shairi hili. (alama 3)
(e) Andika ubeti wa tatu kwa lugha ya nathari. (alama 4)

**5 USHAIRI (alama 20)**

**UTU NI NINI?**

Utu na ubinadamu, ni kama yai na kuku
Utu ni ile nidhamu, Mola aliyokhuluku
Ubinadamu ni damu, ya utu wa kila siku.
Utu wowote wa mtu, ni kuwajali wenzake

Ye yote mwanaadamu, ana asili ya utu.
Ya'ni kwenye yake damu, hakikosi hiki kitu.
Utu sifa maalumu, ya mtu kuitwa mtu,
Utu wowote wa mtu, ni kuwajali wenzake

Utu ni kiumbe hai, tunacho chaonekana
Utu kamwe haudai, tabia ya kujivuna.
Utu ni ule uhai, ushikao uungwana,
Utu wowote wa mtu, ni kuwajali wenzake

Utu huweza pimika, kwa hisia ya akili.
Huweza kuhifadhika, kulingana na fadhili
Utu huweza pendeka, palipo na maadili
Utu wowote wa mtu, ni kuwajali wenzake

Utu unayo aibu, na tabia ya muhali
Utu huenda na jibu, la Imani na ukweli,
Utu huiona tabu, tabia ya ujahili,
Utu wowote wa mtu, ni kuwajali wenzake

Filosofia ya utu, inapinga ubinafsi.
Utu hautaki kitu, cha upeke wa nafsi.

**CONTACT US ON:**
**WhatsApp/Call or Text 0724351706/0726960003**
**EMAIL: Goldlitepublishers@gmail.com**

Utu hauna kiatu, cheupe au cheusi.
Utu wowote wa mtu, ni kuwajali wenzake.

Utu wa kweli kwa mja, ni wenzake kuwajali,
Utu huiona haja, ya kujua watu hali,
Utu ni kuwa pamoja, kwenye shida mbalimbali.
Utu wowote wa mtu, ni kuwajali wenzake.

Utu ni ubinaadamu, udugu na wenzi wako,
Utu wote waheshimu, kwa nidhamu na kicheko
Utu ona mwanadamu, sijitenge peke yako.
Utu wowote wa mtu, ni kuwajali wenzake

Ingawaje tu dhaifu, katika ubinafsi.
Utu kweli nausifu, ubinadamu halisi.
Utu ni sifa tukufu, iletayo kila nemsi
Utu wowote wa mtu, ni kuwajali wenzake

a) Tambua aina ya shairi hili kwa kutolea ithibati (alama 2)
b) Taja sifa tano za mtu mwenye utu kulingana na shairi (alama 5)
c) Tambua mbinu mbili za kimtindo zilizotumiwa na mshairi (alama 2)
d) Ainisha shairi hili kwa kuzingatia vigezo vifuatavyo. (alama 3
i) vipande
ii) vina
iii) mpangilio wa maneno
e) Tambua nafsineni katika shairi hili (alama 1)
f) Tambua mbinu alizotumia mshairi ili kutimiza mahitaji ya kiarudhi (alama 3)
g) Andika ubeti wa saba kwa lugha nathari (alama 4)

**SEHEMU YA D: HADITHI FUPI. MAPAMBAZUKO YA MACHWEO**

**JIBU SWALI LA 6 AU 7**

**6**. (a) "Nilidhani wewe ni rafiki wa dhati, kumbe hasidi mkubwa …"
i) Eleza muktadha wa dondoo hili (alama 4)
ii) Bainisha toni katika dondoo hili (alama 2)
iii) Fafanua sifa sita za mhusika anayesema maneno haya (alama 6)
b) Kwa kurejelea hadithi ya mapambazuko machweo jadili suala la unafiki (alama 8)

**7. KIFO CHA SULUHU**

Mume wangu, hebu zivute fikra zako miaka kumi na mitano iliyopita tulipoingia katika mkataba wa ndoa. Kwa nini unataka kujitia hamnazo kuhusu ahadi ulizozitoa? Umesahau namna tulivyohangaika, tukachekwa na watu, tukakosa hata marafiki na hatimaye tukabandikwa majina ya ajabu? Umesahau, mume wangu? Umesahau namna kazi yako ya

**CONTACT US ON:**
**WhatsApp/Call or Text 0724351706/0726960003**
**EMAIL: Goldlitepublishers@gmail.com**

kuuza makaa ilivyofika hatima ya ghafla baada ya serikali kupiga marufuku ukataji wa miti katika eneo la Dafrao? Naomba ukumbuke. Ninaamini huenda umesahau! Ama cheo chako cha ubunge ulichokipata kwa mbinu nizijuazo mimi kimekulevya na kukufanya uisahau familia yako?

a) Eleza muktadha wa dondoo hili (alama 4)
b) Fafanua mbinu za kimtindo zilizotumika katika dondoo hili. (alama 6)
e) Tambua toni iliyotumika katika dondoo hili. (alama 2)
d) Fafanua umuhimu wa ujumbe alioutoa mnenaji wa maneno haya. Tumia hoja nane(alama 8)

## SEHEMU E: FASIHI SIMULIZI

**8. Soma kifungu hiki kisha ujibu maswali**

Hapo zamani za kale, Nyani na Mamba walikuwa marafiki wa kufa kuzikana. Watoto wao walipendana na kufaana kama ndugu wa toka nitoke. Familia ya Mamba aliishi mtoni nayo ya Nyani aliishi katika msitu uliokuwa maili thelathini kutoka mtoni. Kila mara marafiki hawa walitembeleana na kusaidiana kwa hali na mali. Kwa vile Mamba alikuwa mvuvi msahuhuri, aliweza kumwauni Nyani na aila yake kwa samaki wa aina mbalimbali. Nyani naye alimpelekea Mamba matunda na nafaka kutoka shambani mwake.

Urafiki wao ulikita mizizi na kunawiri zaidi wakati Mamba alipokuja kwa Nyani kumposea mwanawe binti. Ukwe uliutilia viungo uhusiano wa Nyani na Mamba wakawa wanagandana kama kupe na mkia wa Ng'ombe. Wakatenda mengi pamoja. Wakazungumza ya kupwa na ya kujaa. Hakuna hata mmoja wao aliyeutilia shaka uaminifu wa mwenzake. Wake zao nao walifuata kaida ya maji kufuata mkondo. Walikuwa masahibu wa chanda na pete.

Msimu mmoja wa mapukutiko ulishuhudia mabadiliko ya kudumu katika maisha ya Nyani na Mamba. Wakati huo, bahari ilichafuka si haba. Kazi ya Mamba ya uvuvi ikaanza kukabiliwa na majabali ya kila aina. Kila mara Mamba alipokwenda uvuvini, alirudi akichekelewa na nyavu zake. Hakuambulia chochote. Njaa ilianza kubisha hodi katika familia ya Mamba. Hali hii ilitishia kuutia ufa urafiki kati ya Mamba na Nyani. Mamba alivamiwa na pepo ambaye hata yeye alishindwa kumfahamu. Kila mara alipomwona Nyani au watoto wake alitamani kumdakia na kumla mzima mzima. Kadiri aalivyojaribu kujiasa dhidi ya fikira hii mbovu ndivyo moyo wake ulivyoendelea kumshauri, "Una njaa bwana, familia yako itaangamia. Je huoni rafiki yako na familia yake wanaweza kuwa kitoweo? Utaendelea kula wishwa hadi lini? Mbona huyo Nyani ambaye anajiita rafiki yako sasa amekata guu humu? Mbona haji tena kukutazama? Hata karafuu alizokuwa akikuletea ameacha kuleta. "Mamba akaanza kumshuku rafiki yake na akasadiki kuwa Nyani alikuwa mla naye tu.

Usiku mmoja baada ya kula mate na kujilaza kitandani mwake akihesabu nyota, wazo lilimjia. Alikata shauri kumlaghai rafiki yake wa miaka mingi ilia pate kujiokoa yeye na familia yake kutoka katika kinamasi cha njaa. Asubuhi yake alikwenda kwa Nyani akiwa amejinamia kwa jitimai. Alisema, "Rafiki yangu, jana tulipoagana nilipata tanzia. Mjumbe kutoka kijijini aliniarifu kuwa baba yangu ni mgonjwa mahututi. Alisema kwamba baba ananitaka nyumbani upesi," Habari hizi zilimtia Nyani majonzi makuu. Alimwahidi Mamba

**CONTACT US ON:**
**WhatsApp/Call or Text 0724351706/0726960003**
**EMAIL: Goldlitepublishers@gmail.com**

kwamba wangeandamana pamoja. Kwa vile Nyani hangeweza kutembea majini, ilibidi abebwe na Mamba. Alipatwa na kichefuchefu na manyezi kila alipotazama bahari iliyojitandaza mbele yao kwa mbwembwe. Hata hivyo, Mamba alimhakikishia kuwa wangefika salama. Naye kwa Imani iliyotokana na urafiki na mazoea ya miaka mingi, alitulia.

Safari ilikuwa ndefu na yenye machovu yaliyomfanya Nyani kulala mgongoni mwa Mamba. Walipofika kwenye vina vya maji, Mamba aliamua kumpasulia mbarika Nyani. "Rafiki yangu, nimekuwa nikidhani wewe ni rafiki wa dhati, kumbe uzuri wako wa mkakasi? Mimi na wanangu tumetafunwa na njaa kwa miezi kadha sasa huku maghala yako yakishiba na kutapika chakula. Hujadiriki hata siku moja kuja kujua kama nimepata hata senti moja ya kusagia mkunguni. Jana usiku nilipokuwa nikiwazia hali yangu, nilioteshwa katika ndoto kwamba kama ningepata moyo wako na kuula, basi hali ya uhitaji ingeniishia. Moyo wangu unaniuma sana kukufanyia tendo hili, hata hivyo lisilo budi hutendwa."

Nyani alipigwa na butwaa nusura moyo wenyewe ujikabidhi kwa Mamba. Hata hivyo, akili yake nyepesi ilifanya kazi. Alimwambia Mamba,"Ndugu yangu, pole sana ikiwa umekuwa unadhani sikujali. Kwa kweli, hata ungeniomba moyo wangu siku hizo ningekupa tu. Unajua tena sisi Nyani, Tumbili na Kima tuna mioyo mingi. Hata hivyo, nasikitika kuwa Mungu alituambia kuwa daima mioyo yetu itakaa mitini. Basi ndugu mpenzi, badala ya kuendelea na safari hii, turudi pale mtini nikupe moyo wangu pamoja na mitatu ya wanangu kusudi uwalishe wanao na mkeo."

Mamba akaingia mtegoni. Wakarudi hadi ufuoni. Kwa vile Mamba hakuweza kutoka majini, alibaki ufuoni akimngojea rafiki yake amletee mioyo.

Mamba alitunga macho yake kwenye ujia alioufuata Nyani akiomba pasitokee lolote la kumcheleweshа Nyani. Matumbo yalimnguruma kwa njaa. Roho ikampapa kwa tumaini. Alingoja, akongoja, akangoja... wiki, mwezi, mwaka... Nyani hakurudi. Mamba akajua amepwaguliwa na Nyani. Akaapa kumtafuta kwa udi na ambari. Huo ukawa mwisho wa urafiki kati ya Nyani na Mamba. **Hadithi yangu inaishia hapo.**

**Maswali**

a) Tambua kipera cha utungo huu. Thibitisha. (alama 2)

b) Tambua mbinu **sita** kimtindo alizotumia mtambaji wa utungo huu. (alama 6)

c) Umepewa jukumu la kutamba ngano hii. Fafanua mambo **matano** muhimu utakayozingatia ili kufanikisha uwasilishaji wako. (alama 5)

d) Fafanua umuhimu wa ngano hii katika jamii. (alama 3)

e) Kwa kutoa hoja **nne** jadili umuhimu wa maneno yaliyokolezwa rangi katika utambaji wa ngano kama hizi. (alama4)

# GOLDLITE ONLINE SUPPLIES

***Hati ya kuhitimu kisomo cha sekondari kenya(kcse)***

# MTIHANI WA PAMOJA YA CRESCENDO 2025

**102/3**
**KISWAHILI**
**FASIHI.**
**Muda : Saa 2 ½**

**KIDATO CHA NNE**

***Hati ya Kuhitimu Kisomo cha Sekondari Kenya (K.C.S.E)***

***MAAGIZO:***

a) *Andika jina lako na nambari yako ya mtihani katika nafasi ulizoachiwa hapo juu.*
b) *Tia sahihi yako kisha uandike tarehe ya mtihani katika nafasi ulizoachiwa hapo juu.*
c) *Jibu maswali **manne** pekee.*
d) *Swali la **kwanza** ni la **lazima.***
e) *Maswali hayo mengine matatu yachaguliwe kutoka sehemu nne zilizobaki; yaani; Riwaya, Tamthilia, Ushairi, Hadithi Fupi .*
f) *Majibu yote **lazima** yaandikwe kwa lugha ya Kiswahili*
g) *Karatasi hii ina kurasa **6** zilizopigwa chapwa*
h) *Watahiniwa ni **lazima** wahakikishe kwamba kurasa zote za karatasi hii zimepigwa chapa sawasawa na kuwa maswali yote yamo.*

***<u>KWA MATUMIZI YA MTAHINI PEKEE.</u>***

| Swali | Upeo | Alama |
|---|---|---|
| 1 | 20 | |
| | 20 | |
| | 20 | |
| | 20 | |
| Jumla | 80 | |

**CONTACT US ON:**
WhatsApp/Call or Text 0724351706/0726960003
EMAIL: Goldlitepublishers@gmail.com

## SEHEMU A:FASIHI SIMULIZI (ALAMA 20)

**1. LAZIMA**

Hamkuona jinsi tulivyowapiga mabao
Hamkuona vile tuliwachezea kama watoto,tuliwachenga kila mara
Hamkuona waliponea tundu la sindano tungewapiga mabao kumi na mbili
Ingekuwaje timu mbovu kama hii kucheza na miamba kama sisi?
Niliwafunga baada ya sekunde wakati ule nitashindwaje leo?

**Maswali**

a) i)Tambua kipera kinachodokezwa na maelezo haya na ukifafanue. (alama 2)

ii) Fafanua sifa zozote sita za kipera ulichotambua katika (a) (alama 6)

b) i) Wewe ni miongoni mwa wale wanaotambiwa ngano katika kikao cha utambaji wa ngano.Fafanua mambo sita ambayo unaweza kuchangia ili kufanikisha uwasilishaji wa utambaji. (alama 6)

ii) Umeanza mikakati ya kukusanya data kupitia mbinu ya mahojiano. Eleza changamoto sita ambazo unaweza kukumbana nazo nyanjani. (alama 6)

# SEHEMU B:TAMTHILIA

## Timothy M.Arege :Bembea ya Maisha

*Jibu swali swali la 2 au la*

2. Mama!Mamangu mzazi ni mboni ya jicho kwetu.Ananihitaji kipindi hiki cha lala salama.

a) Eleza muktadha wa dondoo hili. (alama 4)

b) Tambua mbinu tatu za lugha zinazojitokeza katika dondoo hili. (alama 3)

c) Fafanua sifa za mhusika '***mamangu mzazi'*** ukirejerea tamthlia nzima. (alama6)

d)Fafanua majukumu ya elimu katika jamii kwa mujibu wa tamthlia ya Bembea ya Maisha. (alama 7)

***au***

3. "Sara: Si neno mama!(kimya).Hakuna kizuri kijacho kwa urahisi.Mazuri hutoka mbali na wakati mwingine yana hadithi za kutisha.Maisha yetu ni mfano wa mbegu iliyopandwa .Mbegu hiyo haina budi kuoza kwanza ndipo ioteshe mche upendezao."

a) Changanua mtindo katika dondoo hili. (alama 8)

b) "Sasa hali ni tofauti. T<u>amaduni,mila na desturi</u> zetu zimezidi kuyakubali mabadiliko."

i) Eleza nafasi ya msemaji wa kauli katika (b),katika kuendeleza tamthilia husika. (alama 6)

ii) Wahusika mbalimbali katika tamthilia ya *Bembea ya Maisha* wamebuni mikakati mwafaka ili kujikomboa kutokana na kauli zilizopigiwa mstari.Fafanua mikakati **sita** kutoka tamthliani. (alama 6)

## SEHEMU C: RIWAYA

### Clara Momanyi: Nguu za Jadi

### Jibu swali la 4 au 5

4. Hakujua akimbilie wapi.Sasa afanye nini?Alilitupia lile jinyama lakini likahepa.Alihisi maisha yake yamo hatarini.

a) Yaweke maneno haya katika muktadha wake. (alama 4)

b) Kwa kutoa mfano,tambua mbinu mbili za lugha katika dondoo hili (alama2)

c) Fafanua umuhimu wa mandhari katika riwaya hii. (alama 6)

d) Jamii ya nchi ya Matuo imesheheni vikwazo ambavyo vinakaa kama nguu,na kutoka jadi nguu hizi zimeathiri kwa upana usawa katika jamii.Tathmini kauli hii kwa hoja **sita.** (alama 6)

***au***

5. Hivyo,alitaka kubadili hali hata kama ilimaanisha kukitia kichwa chake kinywani mwa simba. <u>Alitaka kuliokoa jahazi lililokuwa likielekea mwambani kwa kasi.</u> Lakini angeliweza vipi kupambana na utandu wa mahasidi hao?

a) ) Fafanua umuhimu wa anayerejelewa dondooni katika kukuza na kuendeleza vitushi riwayani. (alama 4)

b) Eleza sababu za mrejelewa kutaka kufaulisha kauli iloyopigiwa mstari. (alama 10)

c) Mwandishi wa riwaya ya Nguu za Jadi amefanikiwa kutumia **mbinu ya majazi** katika kukuza wahusika na mandhari mbalimbali riwayani.Fafanua kwa kutolea mifano **sita**. (alama 6)

## SEHEMU D: USHAIRI

**Jibu Swali la 6 au 7**

6. *Soma shairi lifuatalo kisha ujibu maswali.*

**<u>Barabara.</u>**

Barabara bado ni ndefu
Nami tayari nimechoka tiki
Natamani kuketi
Ninyooshe misuli
Nitulize akili

Lakini

Azma yanisukuma
Mbele ikinihimiza kuendelea
Baada ya miinuko na kuruba
Sasa naona unyoofu wake
Unyoofu ambao unatisha zaidi.

Punde natumbukia katika shimo
Nahitaji siha zaidi ili kupanda tena,
Ghafla nakumbuka ilivyosema
Ile sauti zamani kidogo
“Kuwa tayari kupanda na kushuka”.

Ingawa nimechoka
Jambo moja li dhahiri
Lazima niifuate barabara
Ingawa machweo yaingia
Nizame na kuibuka

Nipande na kushuka

CONTACT US ON:
WhatsApp/Call or Text 0724351706/0726960003
EMAIL: Goldlitepublishers@gmail.com

Jambo moja nakumbuka: Mungu
Je, nimwombe tena?  Hadi lini?
Labda amechoshwa na ombaomba zangu
Nashangaa tena!

Kitu kimoja nakiamini
Lazima niendeleee kujitahidi kwa kila hatua mpya
Nijikokote kuiandama hii barabara yenye ukungu
Nikinaswa na kujinasua,
Yumkini nitafika mwisho wake
Ikiwa wangu mwisho haitauwahi kabla.  ***(Timothy Arege)***

**<u>Maswali:</u>**

(a) Taja aina ya shairi hili. (alama 2)
(b) Eleza toni ya shairi hili. (alama 2)
(c) Fafanua dhamira ya shairi hili. (alama 2)
(d) Bainisha vipengele vifuatavyo vya kimtindo katika shairi hili. (alama 3)
(i) Tanakuzi
(ii) mbinu rejeshi
(iii) Taswira
(e) Eleza umuhimu wa maswali balagha katika shairi. (alama 2)
(f) Andika ubeti wa mwisho kwa lugha nathari. (alama 4)
(g) Eleza matumizi ya mistari mishata katika shairi hili. (alama 2)
(h) Eleza muundo wa shairi hili. (alama 3)

**AU**

***7. Soma shairi  hili kisha uyajibu maswali;***

Jicho, tavumiliaje, kwa hayo unayo?
Kicho, utasubirije, maonevu yapitayo?
Kwacho, lijalo nalije, nimechoka vumiliyo
Naandika!

Moyo, unao timbuko, maudhi tusikiayo
Nayo, visa na mauko, wanyonge yawakutayo,
Kwayo, sina zuiliko, natoa niyahisiyo
Naandika!

Hawa, wanatumuliya, dhiki wavumiliayo
Hawa, mamiya, na mali wazalishayo
Hawa, ndo wanaumiya, na mafia wakutayo
Naandika!

Hawa, sioni wengine, kwao liko angamiyo
Hawa, huwapa unene, watukufu wenye nayo

Hawa, bado ni wavune, kwa shida waitikayo
Naandika!

Bado, wawapo mabwana, wenye pupa na kamiyo
Bado, tofauti sana, kwa pato na mengineyo
Bado, tuling'owe shina, ulaji pia na choyo.
Naandika!

**Maswali**

a) Malenga wa shairi hili alidhamiria kufafanua masuala kadhaa yanayokumba Jamii.Taja **manne** ya masuala haya kwa kurejerea shairi. (alama 4)

b) Tambua bahari za shairi hili kwa kuzingatia vigezo vifuatavyo; (alama 4)

i) vina
ii) kibwagizo
iii) idadi ya vipande
iv) mishororo

c) Kwa kutoa mifano,tambua mbinu **mbili** ambazo mshairi ametumia kutosheleza mahitaji ya kiarudhi. (alama2)

d) Tambua kwa mifano mbinu **mbili** za kimtindo alizotumia mshairi. (alama4)

e) Andika ubeti wa **nne** katika lugha nathari. (alama 4)

f)Tambua na ueleze toni katika shairi hili. (alama 2)

## SEHEMU E: HADITHI FUPI

**D.Lutomia na Phibbian Muthama:** *Mapambazuko ya Machweo na Hadithi Nyingine*

8.***Fadhila za Punda***

Alipozidiwa akapoteza fahamu.Fahamu zilipomrudia,maumivu yakamvamia.Mumewe hakuonekana,amejiendea na kumwaacha afilie mbali.Alilia machozi yakamwisha.

a)Eleza muktadha wa dondoo hili. (alama 4)

b)Taja mbinu **mbili** za lugha zilizotumika katika dondoo hili. (alama 4)

c)Fafanua mbinu **nne** za kutambua sifa za mhusika anayerejelewa. (alama 4)

d)Kwa kurejelea hadithi "Fadhila za punda" onyesha kwa hoja **nane** ufaafu wa mdokezo wa methali ufuatao: ***maskini akipata makalio hulia bwata*** kwa kutolea mifano mwafaka hadithini. (alama 8)

**GOLDLITE ONLINE SUPPLIES**

**MTIHANI WA PAMOJA WA SHULE ZA KITAIFA**

***Hati ya kuhitimu kisomo cha sekondari***

---

**Jina ………………………………………….……… Nambari………………………………………**

**Sahihi ………………….…...………………….............Tarehe……………………………………......**

---

# MTIHANI WA PAMOJA WA EAGLES

**KISWAHILI**

**KARATASI YA TATU (FASIHI)**

**KIDATO CHA NNE**

**MUDA: Saa 2 Dakika 30**

**MAAGIZO :**

***a)*** *Jibu maswali manne pekee.*

***b)*** *Swali la* **kwanza** *ni la lazima.*

***c)*** *Maswali hayo mengine matatu yachaguliwe kutoka sehemu nne zilizobaki;yaani ;Riwaya, tamthilia, hadithi fupi na fasihi simulizi.*

***d)*** *Usijibu maswali mawili kutoka sehemu moja*

***e)*** *Majibu yote lazima yaandikwe kwa lugha ya Kiswahili.*

***f)*** *Karatasi hii inakurasa 7 zilizopigwa chapa.*

***g)*** *Watahiniwa lazima wahakikishe kwamba kurasa zote za karatasi hii zimepigwa chapa sawasawa na kuwa maswali yote yamo*

**CONTACT US ON:**
WhatsApp/Call or Text 0724351706/0726960003
EMAIL: Goldlitepublishers@gmail.com

**SEHEMU A : SWALI LA LAZIMA (ALAMA 20)**

**1. USHAIRI**

**UTU NI NINI ?**

Utu na ubinadamu, ni kama yai la kuku
Utu ni ile nidhamu,Mola aliyokhuluku
,ubinadamu ni Damu,ya utu wa kila siku
Utu wowote wa mtu,ni kujali mwenzake.

Ye yote mwanaadamu, ana asili ya utu,
Ya'ni kwenye yake damu, hakikosi hiki kitu
Utu sifa maalum, ya mtu kuitwa mtu,
Utu wowote wa mtu, ni kujali mwenzake

Utu ni kiumbe hai, tunacho chaonekana
Utu kamwe haudai, tabia ya kujivuna,
Utu ni ule uhai, ushikao uungwana,
Utu wowote wa mtu, ni kuwajali wenzake

Utu huweza pimika, kwa hisia ya akili,
Huwezi kuhifadhika, kulingana na Fadhili,
Utu huweza pendeka, palipo na maadili
Utu wowote wa mtu, ni kuwajali wenzake

Utu unayoaibu, na tabia ya muhali,
Utu huenda na jibu, la Imani na ukweli,
Utu huiona tabu, tabia ya ujahili,
Utu wowote wa mtu ni kuwajali wenzake

Filosofia ya utu, inapinga ubinafsi,
Utu hautaki kitu, cha upeke wa nafsi,
Utu hauna kiatu, cheupe au cheusi
Utu wowote wa mtu, ni kuwajali wenzake

Utu wa kweli kwa mja, ni mwenzake kuwajali,
Utu huinoa haja, ya kujua watu hali,
Utu ni kuwa pamoja, kwenye shida mbalimbali
Utu wowote wa mtu, ni kuwajali wenzake

Utu ni ubinaadamu, udugu na wenzi wako,
Utu wote waheshimu, kwa nidhamu na kicheko,
Utu ona mwanadamu, sijitenge peke yako,
Utu wowote wa mtu,ni kuwajali wenzake

Ingawaje tu dhaifu, katika ubinafsi,
Utu kweli nausifu, ubinadamu halisi,
Utu ni safi tukufu, iletayo kila nemsi,
Utu wowote wa mtu, ni kuwajali wenzake

**CONTACT US ON:**
WhatsApp/Call or Text 0724351706/0726960003
EMAIL: Goldlitepublishers@gmail.com

a. Tambua aina ya shairi hii kwa kutolea ithibati. (Alama 2)

b. Taja sifa tano za mtu mwenye utu kulingana na shairi. (Alama 5)

c. Tambua mbinu mbili za kimtindo zilizotumiwa na mshairi. (Alama 2)

d. Ainisha shairi hili kwa kuzingatia vigezo vifuatavyo. (Alama 3)

I. Vipande
II. Vina
III. Mpangilio wa maneno

e. Tambua nafsineni katika shairi. (Alama 1)

f. Tambua mbinu tatu alizotumia mshairi ili kukidhi mahitaji ya kiarudhi. (Alama 3)

g. Andika ubeti wa saba kwa lugha ya nathari. (Alama 4)

## SEHEMU B : RIWAYA

**Nguu za Jadi :** *Clara Momanyi*

Jibu swali la 2 au 3

2. ‘’Aah, si unajua wale watu hatari. Lakini hawatakuwa na nguvu tena. Njia zao zote nitazifunga…”

a. Eleza muktadha wa dondoo hili. (Alama 4)

b. Jadili hatari zilizosababishwa na watu wanaorejelewa na msemaji. (Alama 10)

c. Msemaji ananuia kuzifunga njia za warejelewa vipi? (Alama 6)

3. Fafanua sifa na umuhimu wa wahusika wafuatao. (Alama 20)

a. Sihaba

b. Mwamba

c. Mrima

d. Chifu Mshabaha

## SEHEMU C TAMTHILIA

*T. Arege*: **Bembea ya Maisha**

Jibu swali la 4 au la 5

‘’…wakati mwingine mwindaji huwa mwindwa. Hata kijijini wanaishi watu. Watu hao hawakumbwi na dhiki kiasi hiki. Ya nini kung’ang’ana kuyatafuta Maisha kama kwamba hayapatikani?Maisha mshumaa uso mkesha!Ukijiachia sana peupe hata upepo unaweza kuumiza kabla ya Kulika hadi nchani.”

**Maswali**

4.

a. Eleza muktadha wa dondoo hili. (Alama 4)

b. Bainisha toni katika kauli hili. (Alama 2)

c. Eleza vipengele vinne vya kimtindo alivyotumia msemaji kufanikisha uwasilishaji wa ujumbe. (Alama 4)

d. Eleza umuhimu wa msemaji katika kuendeleza ploti ya tamthilia hii. (Alama10)

5.

a. Fafanua umuhimu wa mazungumzo kati ya Luka, Beni na Yona katika kujenga tamthilia ya ‘’Bembea ya Maisha.” (Alama 10)

b. ‘’Bembea inapolika na kukatika haiwi mwisho wa michezo.Huungwa na mchezo kwanza tena.’’Thibitisha ukweli wa kauli hii kwa kutolea mifano mwafaka tamthiliani. (Alama 10)

**SEHEMU YA C**

***Hadithi Fupi – Mapambazuko Ya Machweo Na Hadithi Nyingine – Dw Lutomia***

***Jibu swali la sita au la saba***

6. Jadili maudhui ya taasubi ya kiume katika hadithi ya fahila za punda. (Alama 20)

7. Jadili shida zilizowakumba raia wa matopeni katika hadithi ya msiba wa kuitakia ya D.W. Lutomia. (Alama 20)

**SEHEMU D: FASIHI SIMULIZI**

8. **Soma kifungu hiki kisha ujibu maswali.**

Hapo zamani za kale, Nyani na mamba walikuwa marafiki wa kufa kuzikana. Watoto wao walipendana na kufaana kama ndugu wa toka nitoke. Familia ya mamba aliishi mtoni nayo ya Nyani aliishi katika msitu uliokuwa maili thelathini kutoka mtoni. Kila mara marafiki hawa walitembeleana na kusaidiana kwa hali na mali. Kwa vile mamba alikuwa mvivu msahuhuri, aliweza kumwauni Nyani na aila yake kwa Samaki wa aina mbalimbali. Nyani naye alimpelekea mamba matunda na nafaka kutoka shambani mwake.

Urafiki wao ulikita mizizi na kunawiri zaidi wakati mamba alipokuja kwa Nyani kumposea mwanawe binti. Ukwe uliutilia viungo uhusiano wa Nyani na mamba wakawa wanagandana kama kupe na mkia wa ng’ombe. Wakatenda mengi Pamoja. Wakazungumza ya kupwa na ya kujaa. Hakuna hata mmoja wao aliyeutilia shaka uaminifu wa mwenzake. Wake zao nao walifuata kaida ya maji kufuata mkondo. Walikuwa masahibu wa chanda na pete. Msimu mmoja wa mapukutiko ulishuhudia mabadiliko ya kudumu katika maisha ya Nyani na mamba. Wakati huo, bahari ilichafuka si haba. Kazi ya mamba ya uvivu ikaanza kukabiliwa na majabali ya kila aina. Kila mara mamba alipokwenda uvuvini, alirudi akichekelewa na nyavu zake. Hakuambulia chochote. Njaa ilianza kubisha hodi katika familia ya mamba. Hali hii ilitishia kuitia ufa urafiki kati ya mamba na Nyani. Mamba alivamiwa na pepo ambaye hata yeye alishindwa kumfahamu. Kila mara alipomwona. Nyani au Watoto wake alitamani kumdakia na kumla mzima mzima. Kadiri kujiasa dhidi ya fikira hii mbovu ndivyo moyo wake ulivyo endelea kumshauri, ‘’ Una njaa bwana, familia yako itaangamia. Je huoni rafiki yako na familia yake wanaweza kuwa kitoweo ?

Utaendelea kula wishwa hadi lini? Mbona huyo Nyani ambaye alijiita rafiki yako sasa amekata guu humu? Mbona haji tena kukutazama hata karafu alizokuwa akikuletea ameacha kuleta.'' Mamba akaanza kumshuku rafiki yake na akasadiki kuwa nyali alikuwa mla naye tu. Usiku mmoja baada ya kula mate na kujilaza kitandani mwenzake akihesabu nyota, wazo lilimjia. Alikata shauri kumlaghai rafiki yake wa miaka mingi iliapate kujiokoa yeye na familia yake kutoka katika kinamasi cha njaa. Asubuhi yake alikwenda kwa Nyani akiwa amejinamia kwa jitimai. Alisema, ''Rafiki yangu, jana tulipoagana nilipata tanzia. Mjumbe kutoka kijijini aliniarifu kuwa baba yangu ni mgonjwa mahututi. Alisema kwamba baba ananitaka nyumbani upesi,'' Habari hizi zilimtia Nyani majonzi makuu. Alimwahidi mamba kwamba wangeandamana Pamoja. Kwa vile Nyani hangeweza kutembea majini ilibidi abebwe na mamba. Alipatwa na kichefuchefu na manyezi kila alipotazama Bahari iliyojitandaza mbele yao kwa mbwembwe. Hata hivyo, mamba alimhakikishia kuwa wangefika salama. Naye kwa Imani iliyotokana na urafiki na mazoea ya miaka mingi, alitulia.

Safari ilikuwa ndefu na yenye machovu yaliyomfanya Nyani kulala mgongoni mwa mamba. Walipofika kwenye vina vya maji, mamba aliamua kumpasulia mbarika Nyani. ''rafiki yangu,nimekuwa nikidhani wewe ni rafiki wa dhati,kumbe uzuri wako wa mkakasi?mimi na wanangu tumetafuna na njaa kwa miezi kadha sasa huku maghala yako yakishiba na kutapika chakula. Hujadhiriki hata siku moja kuja kujua kama nimepata hata senti moja ya kusagia mkunguni. Jana usiku nilipokuwa nikiwazia hali yangu, nilioteshwa katika ndoto kwamba kama ningepata moyo wako na kuula, basi hali ya uhitaji ingeniishia. Moyo wangu unaniuma sana kukufanyia tendo hili, hata hivyo nilisobudi hutendwa''

Nyani alipigwa na butwaa nusura moyo wake mwenyewe ujikabidhi kwa mamba. Hata hivyo, akili yake nyepesi ilifanya kazi. Alimwambia mamba, '' ndugu yangu, pole sana ikiwa umekuwa unadhani sikujali. Kwa kweli, hata ungeniomba moyo wangu siku hizo ningekupa tu. Umejua tena sisi Nyani, tumbili na kima tuna mioyo mingi. Hata hivyo nasikitika kuwa Mungu alituambia kuwa daima mioyo yetu itakaa mitini. Basi ndugu mpenzi, badala ya kuendelea na safari hii, turudi pale mtini nikupe moyo wangu pamoja na mitatu ya mwanangu kusudi uwalishe wanao na mkeo.'' Mamba akaingia mtegoni. Wakarudi hadi ufuoni. Kwa vile mamba hakuweza kutoka majini, alibaki ufuoni akimngojea rafiki yake amlete mioyo.

Mamba alitunga macho yake kwenye ujia alioufuata Nyani akiomba pasitokee lolote la kumchelewesha Nyani. Matumbo yalimguruma kwa njaa. Roho ikampapa kwa tumaini. Alingoja, akongoja,akangoja…wiki,miezi,mwaka… Nyani hakurudi. Mamba akajua amepwaguliwa na Nyani. Akaapa kumtafuta kwa udi na ambari.huo ukawa mwisho wa urafiki kati ya Nyani na mamba. **Hadithi yangu inaishia hapa.**

**Maswali**

a. Tambua kipera cha utungo huu. Thibitisha. (Alama 2)

b. Tambua mbinu sita kimtindo alizotumia mtambaji wa utungo huu. (Alama 6)

c. Umepewa jukumu la kutamba ngano hii. Fafanua mambo Matano muhimu utakayozingatia ili kufanikisha uwasilishaji wako. (Alama 5)

d. fafanua umuhimu wa ngano hii katika jamii. (Alama 3)

e. Kwa kutoa hoja nne jadili umuhimu wa maneno yaliyokolezwa rangi katika utambaji wa ngano kama hizi. (Alama 4)

**CONTACT US ON:**
WhatsApp/Call or Text 0724351706/0726960003
EMAIL: Goldlitepublishers@gmail.com

# GOLDLITE ONLINE SUPPLIES

*Cheti cha Kuhitimu Kisomo cha Sekondari*

**TATHMINI YA MAJARIBIO (I), 2025**

**102/3 Kiswahili - Fasihi Karatasi ya 3**

**KIDATO CHA NNE 2025 Saa: 2½**

# SHULE YA UPILI YA KENYA HIGH

**Jina: ……………………………………Nambari: …………..Tarehe……..................**

**Mkondo:………… Shule:..................................................Sahihi:………..................**

**Maagizo**

- a) *Andika jina lako, nambari ya usajili, mkondo, sahihi na tarehe katika nafasi ulizoachiwa hapo juu.*
- b) *Jibu maswali manne pekee.*
- c) *Swali la kwanza ni la lazima.*
- d) *Maswali hayo mengine matatu yachaguliwe kutoka sehemu nne zilizobaki; Riwaya, Hadithi Fupi, Ushairi na Fasihi simulizi*
- e) *Usijibu maswali mawili kutoka sehemu moja.*
- f) *Karatasi hii ina kurasa 18. Watahiniwa ni lazima wahakikishe kwamba kurasa zote za karatasi hii zimepigwa chapa sawasawa na kuwa maswali yote yamo.*

**Kwa matumizi ya mtahini pekee**

| SWALI | UPEO | ALAMA |
|---|---|---|
| 1 | 20 | |
| | 20 | |
| | 20 | |
| | 20 | |
| JUMLA | 80 | |

**CONTACT US ON:**
**WhatsApp/Call or Text 0724351706/0726960003**
**EMAIL: Goldlitepublishers@gmail.com**

## SEHEMU YA A: USHAIRI

**1. Lazima**

**Soma shairi lifuatalo kisha ujibu maswali**

Jiulize ni kwa nini, uanzapo kuongea
Sana sana makundini, watu hukuondokea
Ndugu ujitathmini, hakika umepotea
Sisi twakuombea, mwenye damu ya kunguni!

Mwenye damu ya kunguni, nayo lugha ya ajuza
Wengi hawamtamani, maneno yake yaliza
Yeye ana walakini, dosari kuliko pweza
Kama wewe umefunza, sote hutuona duni!

Sote hutuona duni, na hilo tumezowea
Kazi zetu zote guni, yeye tu amebobea
Umewachokoza mbuni, mateke anapokea
Sisi twakuombea, upae hadi hewani!

Upae hadi hewani, ujione kama bingwa
Mewashinda gazetini, wandishi kwako wapingwa
Yeye kwetu mpinzani, metia mipaka tingwa
Twakuombea mtafiti, hesabu hadi mizani!

Hesabu hadi mizani, utunge kwa kukosoa
U hodari hesabuni, nasi tushakuzoea
We nduli kwa majirani, na waja mekutegea
Kurekebisha hujui, ywatanika peupeni!

Ywatanika peupeni, ywajisifu mjuaji
Amezidi zetu mboni, na amejivunjia mji
Twamwachia waamuzi, kesi wasome majaji
Sisi twakuombea, sirekebike kidogo!

**CONTACT US ON:**
**WhatsApp/Call or Text 0724351706/0726960003**
**EMAIL: Goldlitepublishers@gmail.com**

**Maswali**

**(a)** Eleza ujumbe unaojitokeza katika shairi hili **(alama6)**

**(b)** Tambua miundo wa shairi hili **(alama4)**

**(c)** Tambua bahari ya shairi hili kwa kuzingatia mpangilio wa maneno **(alama2)**

**(d)** Andika ubeti wa tatu kwa lugha nathani **(alama4)**

**(e)** Tambua aina tatu za takriri zinazojitokeza **(alama3)**

**(f)** Onyesha toni ya shairi hili **(alama1)**

**SEHEMU YA B: RIWAYA: NGUU ZA JADI**

**Clara Momanyi:Nguu za jadi**

**Jibu swali la 2 au la 3**

**2. Soma dondoo lifuatalo kisha ujibu maswali yafuatayo:**

"Kisisi kilimvaa. Sasa alikuwa akihema pumzi za mjusi. Jasho lilimtiririka usoni kama aliyemwagiwa maji. Alijikwaa miguu ovyo. Kiwiliwili chake kikaanza kuyumba kwa hofu na hawafu."

**(a)** Tambua aina za taswira katika dondoo hili **(alama4)**

**(b)** Eleza aina mbili za urudiaji katika dondoo **(alama2)**

**(c)** Eleza na uthibitishe mandhari ambamo dondoo hili limetolewa **(alama2)**

**(d)** Eleza toni ya dondoo hili **(alama2)**

**(e)** Eleza umuhimu wa mandhari ya dondoo hili ukirejelea vipengele vifuatavyo**(alama10)**

**(i) Maudhui**

**(ii) Wahusika**

**3.** 'Hakuna siri duniani" Thibitisha dai hili ukirejelea riwaya yote ya Nguu za jadi **(alama20)**

**SEHEMU YA C: TAMTHILIA**

**Timothy M. Arege.:Bembea ya Maisha**

**Jibu swali la 4 au la 4**

**4. (a)Soma dondoo lifuatalo kisha ujibu maswali yafuatayo:**

Ukilazwa tayari unakuwa umeonja seli. Hata wahudumu wenyewe hawana mlahaka mwema. Amri na vitisho kama askari. Unashindwa kama uuguze moyo ama ugonjwa. Katika wodi hewa iliyojaa harufu ya dawa imezagaa, vitanda vimesalimu amri mpaka shiti zikagura. Yaani hali nzima haikupi matumaini ya kutoka ukiwa bora.

a) Changanua mtindo **(alama6)**

b) Asna na Sara ni wahusika wawili wenye mitazamo tofauti kuhusu maisha. Thibitisha (alama6)

c) Jadili changamoto zinazokumba asasi ya ndoa kwa mujibu wa tamthilia ya Bembea ya Maisha **(alama8)**

**5.** Jadili mambo yanayofanikisha ndoa katika tamthilia ya Bembea ya maisha **(alama20)**

**SEHEMU C: HADITHI FUPI**

**CONTACT US ON:**
**WhatsApp/Call or Text 0724351706/0726960003**
**EMAIL: Goldlitepublishers@gmail.com**

**D.W Lutomia na Phibbian Muthama: Mapambazuko ya Machweo na Hadithi Nyingine**

**Jibu swali la 6 au la 7**

6. **Harubu ya Maisha – Paul Ng'ang'a Mutua**
   a) Weka dondoo hili katika muktadha wake (Alama 4)
      *Dondoo "**Naja. Nakamilisha shughuli ndogo hapa kisha nianze safari...**"*
   b) Eleza sifa sita za msemaji wa kauli hii (Alama 6)
   c) Jadili changamoto wanazokumbana nazo waajiriwa kwa kurejelea hadithi hii (Alama 10)
7. **Mzimwi wa Kipwerere**
   (a) Eleza ni kwa nini hadithi fupi ***"Mzimwi wa Kipwerere"*** ikaitwa Mzimwi wa Kipwerere
   (b) Kwa nini mzimu huu unatisha **(alama5)**
   (c) Mzimwi wa Kipwerere ulikuwa na siri yake. Thibitisha **(alama10)**

**SEHEMU YA E: FASIHI SIMULIZI**

8. **Soma utungo ufuatao kisha ujibu maswali yanayofuata**

Katiechi Analia, Katiechi Analia
Chozi lausaliti undani wake
Undani ambao ameuficha kwa miaka na mikaka
Undani ambao japo anachelea kutangaza asije akaonekana apendaye chongo…
Itabidi kuutoa, kuumwaga mtama

Na kiini cha chozi hili ni kwamba imewadia
Imewadia siku ya siku kanisani kwenda,
Kujitia pingu
Kujitia pingu, pingu za aushi
Je, hakuyataka haya?
Hakupania yapakata kama mwanagenzi,
Apatakavyo malaika mikononi pake?
Kwani basi analovya, kidari kwa maji chumvi?
Shavu lake laini,kuwa kijivu kwa shaka?
Ama ni yano mapenzi yalomlemea?
Mapenzi alopalia kwa miaka na dahari?

Kipi kinokwinamisha,
Kwa tewengu kukubwaga?
Ama ni majukumu kuhofia mwenzetu?

**CONTACT US ON:**
**WhatsApp/Call or Text 0724351706/0726960003**
**EMAIL: Goldlitepublishers@gmail.com**

Ni adha za ulezi?
Ni hofu ya kutelekezwa?
Jikoni kuachwa jukumu la kawaida?
Ama ni ugeni kwa nasaba uso asili unokuuguza?
Je, ni mazoea unochelea kuacha?
Ama ni uzito wa nanga ua huba?
Kipi, sema ewe mwenzangu, sema.

Nikahi ni sitara
Usumbufu kuepuka vipanga na mwewe
Ndoa huneemesha na jina kukupa utatukukuka kimwana
Shujaa ukapata wa kukulinda
Miliki ni hakikisho kutoka kwa dume hata katika mauko,
Penzi halali kupata, na warithi kuambulia,
Wa kiume kukufaa
Silie mwana silie,
Watutia simanzi
Waitia ndoa doa, nuksani kukuandamia.

Wavyele mpeni Baraka
Mashangazi mtemeeni mate
Viganjani kumiminia pumzi zenu za neema
Ndoa yake kutengenea
Maumbu acheni
Kulengwa na machozi
Mwamliza zaidi, unyonge kumtia
Baba mtu mshike kondooyo,
Mwongoze kidesturi, madhabahu karibia,
Mkabidhi mkweo, mwenzi wake wa maisha.

Ndiye takayekuwa fahali, simba atakuwa kikaida
Amri tatoa yeye, malkia kufuata,
Utashi wake tatimizwa, ndivyo sheria inenavyo
Bila yeye kutamka mtamba aandamwi na sahibu
Tampenda ewe kinda, tanyenyekea bila kulalama

Penzi talinda wewe, wengine sije paramia

Kukupoka mwamba wako!

**Maswali**

(a) Ainisha utungo huu kimaudhui. **(alama1)**

(b) Eleza sifa tatu za utungo huu **(alama3)**

(c) Chambua mitindo katika utungo huu. **(alama4)**

(d) Unanuia kuwasilisha utungo huu jukwani, tathmini vipengele sita ambavyo

(e) Eleza manufaa manne ya ndoa kutokana na wimbo huu. **(alama4)**

(f) Jamii ina matarajio yepi kuhusu wanandoa? (**alama2)**

**CONTACT US ON:**
**WhatsApp/Call or Text 0724351706/0726960003**
**EMAIL: Goldlitepublishers@gmail.com**

# GOLDLITE ONLINE SUPPLIES

*Hati Ya Kuhitimu Kisomo Cha Sekondari Kenya (Kcse)*

**MITIHANI YA PAMOJA YA SHULE ZA KITAIFA 2025**

**JINA: ……………………………NAMBARI YA USAJILI: ………………………….**

**SAHIHI YA MTAHINIWA: ……………………TAREHE: ……DARASA: …...........**

# SHULE YA UPILI YA KISII

**102/3**
**KISWAHILI**
**FASIHI.**
**Muda : Saa 2 ½**

***MAAGIZO:***

a) *Andika jina lako na nambari yako ya mtihani katika nafasi ulizoachiwa hapo juu.*
b) *Tia sahihi yako kisha uandike tarehe ya mtihani katika nafasi ulizoachiwa hapo juu.*
c) *Jibu maswali **manne** pekee.*
d) *Swali la **kwanza** ni la **lazima.***
e) *Maswali hayo mengine matatu yachaguliwe kutoka sehemu nne zilizobaki; yaani; Riwaya, Tamthilia, Ushairi, Hadithi Fupi .*
f) *Majibu yote **lazima** yaandikwe kwa lugha ya Kiswahili*
g) *Karatasi hii ina kurasa **6** zilizopigwa chapwa*
h) *Watahiniwa ni **lazima** wahakikishe kwamba kurasa zote za karatasi hii zimepigwa chapa sawasawa na kuwa maswali yote yamo.*

***KWA MATUMIZI YA MTAHINI PEKEE.***

| Swali | Upeo | Alama |
|---|---|---|
| 1 | 20 | |
| | 20 | |
| | 20 | |
| | 20 | |
| Jumla | 80 | |

**CONTACT US ON:**
WhatsApp/Call or Text 0724351706/0726960003
EMAIL: Goldlitepublishers@gmail.com

**SEHEMU YA A: USHAIRI SWALI LA LAZIMA.**

**1. Soma shairi lifuatalo kisha ujibu maswali yanayofuata**

a) Mbiu naipulizia, kwa wa hapa na wa ng'ambo,
Kwani ngoja 'mesikia, inaumiza matumbo,
Kwa upole sitafyoa, hata kama kwa kimombo,
Yafaa jihadharia, maisha yas,ende kambo;

b) Maisha yas'ende kombo, kututoa yetu ari,
Zingatia haya mambo, wetu walezi mukiri,
Kuwa wana kwa viambo, huwa Baraka na kheri
Watunzeni na maumbo, msijezusha hatari

c) Msijezusha hatari, na nyingi hizi zahana,
Wazazi haya si siri, mawi mnayoandama
Twaeleza kwa uzuri, matendoyo yatuuma.
Watoto tunayo mori, ni lini mtajakoma?

d) Ni nani mtajakoma, na pombe ziso halali?
Sio baba sio mama, mbona ny'hamtujali
Mwafa ja nzi twasema, mwatuacha bila hali
Hangaiko acha nyuma, kwani hamuoni hili?

e) Kwani hamuoni hili, kila mwapigana
Nyumbanizo hatulali, jehanamu tumeona
Mwatusumbua akili, twaumia tena sana
Achene na ukatili, kwani upendo hamna,

f) Kwani upendo hamna, Kama mbwa mwatuchapa
Mwatuchoma sisi wana, mioyetu yatupapa
Pa kujificha hatuna,tumebaki tukitapa
Maisha hamu hayana, umevunjwa na mifupa.

g) Tumevunjwa na mifupa, hata leo uke wetu,
Mwatubaka na kuapa, kutung'ata nyi' majitu,
Maisha hatujakopa, fahamu mkosa utu,
Hayo makeke na pupa, mtakoma utukutu,

h) Mtakoma utukutu, na kutumia mikiki,
Na tabia zenye kutu, tumechoka nayo chuki,
Hatutakubali katu, kutendewa yenye siki,
Serikali fanya kitu, kwani nasi tuna haki.

**CONTACT US ON:**
WhatsApp/Call or Text 0724351706/0726960003
EMAIL: Goldlitepublishers@gmail.com

*Maswali*

**a)** Eleza dhamira ya mtunzi wa shairi hili. (alama 2)

**b)** Fafanua tamathali nne za usemi zilizotumiwa katika shairi hili. (alama 4)

**c)** Taja nafsi neni katika shairi hili. (alama 1)

**d)** Eleza bahari nne zinazowakilishwa katika shairi hili. (alama 4)

**e)** Andika ubeti wa nne kwa lugha nathari. (alama 4)

**f)** Eleza maudhui matatu yanayojitokeza katika shairi hili. (alama 3)

**g)** Huku ukitoa mfano taja uhuru mmoja wa mshairi ambao umetumiwa katika shairi hili. (alama 2)

## SEHEMU B: TAMTHILIA-BEMBEA YA MAISHA

**Jibu swali la 2 au 3**

**2.** Eleza nafasi ya mbinu rejeshi katika tamthilia ya Bembea ya Maisha kukuza vipengele vifuatavyo:

a) Maudhui (alama 8)

b) Ploti (alama 8)

c) Wahusika (alama 4)

**3.** "Ninavaa vizuri na kujivisha tabasamu ila ndani viraka na huzuni tele"

a) Eleza muktadha wa dondoo hili. (alama 4)

b) Tambua kipengele cha mtindo katika dondoo hili. (alama 2)

c) Tambua sifa za msemewa inayojitokeza katika dondoo hili. (alama 2)

d) Eleza mambo yanayomjaza msemaji viraka na huzuni. (alama 12)

## SEHEMU C:
## HADITHI FUPI: MAPAMBAZUKO YA MACHWEO NA HADITHI NYINGINE

**Jibu swali la 4 au 5**

**4.** "Kwa kweli, nimeungulika sana miaka yote hii kwa unyama tuliomtendea Jack.. ."

a) Eleza muktadha wa dondoo hili. (alama 4)

b) Jadili umuhimu wa msemaji wa dondoo hili. (alama 6)

c) Jadili ukatili aliokuwa ametendewa mhusika jack kulingana na dondoo hili. (alama 5)

d) Kwa kurejelea mhusika jack, jadili maudhari ya nafasi ya vijana. (alama 5)

**5.** Onyesha namna mwandishi wa hadithi ya Nipe Nafasi alivyodokeza maudhui ya taasubi ya kiume. (alama 20)

## SEHEMU YA D: RIWAYA:
## NGUU ZA JADI. CLARA MOMANYI

**Jibu swali la 6 au 7**

6. "Alitazama jinsi kina mama wengine walijikunyata kutokana na kibaridi kile cha asubuhi"

a) Eleza muktadha wa dondoo hili. (al.4)

b) Tambua mbinu ya lugha katika dondoo hili. (al.2)

c) Fafanua umuhimu wa mandhañ ya dondoo hili (al.14)

7. Eleza jinsi Mtemi Lesulia amejenga maudhui mbalimbali katika riwaya ya Nguu za Jadi. (alama 20)

## SEHEMU E: FASIHI SIMULIZI

**CONTACT US ON:**
WhatsApp/Call or Text 0724351706/0726960003
EMAIL: Goldlitepublishers@gmail.com

**8. *Soma hadithi hii kisha ujibu maswali***

Ilikuwa alfajiri yenye baridi. Umande ulitapakaa kote.Ukungu ulitanda hivi kwamba hungeweza kumuonamtu alikuwa hatua chache mbele yako.Ndovu alipoamka, alikuta fisi mlangoni pake. Fisi alikuwa amemlimia ndovu shamba lake, lakini alikuwa hajalipwa ujira wake. Kila alipomwendea ndovu kwa ajili ya malipo yake, fisi alitiliwa huku na kutolewa kule.”Leo ni leo”,fisialimwambiandovu.”Nimevumilia vya kutosha. Kila siku ninapokuja kuchukua pesa zangu, hukosi hadithi mpya ya kunisimulia. Leo sitoki hapa bila pesa zangu!” Fisi alipomaliza kumwaga joto lake,ndovu alimwambia: “Sikiliza fisi. Mimi nimeheshi mika kote kijijini. Naona haja yako ni kunivunjia heshima –mbele ya familia yangu na wanakijiji kwa jumla. Sikulipi pesa zako, mpaka ujifunze kuwaheshimu wazee. Nakuamuru uondoke hapa mara moja, kabla sijakasirika! Nataka uende popote,unapofikiria kwamba unaweza kupata msaada.

Ukienda kwa chifu,usisahau kwamba tunakunywa na yeye. Ukienda polisi, mkuu wa kituo amejaa tele mfukoni mwangu. Ukienda mahakamani, hakimu tulisoma darasa moja. Popote uendapo, hakuna yeyote atakayekusikiliza” “Zaidi ya hayo, hakuna yeyote atakayekuamini.Mimi naitwa Bwana pesa.Kwangu umeota pesa na kustawi. Nani ataamini kwamba naweza kushindwakulipa vijisenti vichache ninavyodaiwa na fisi?”Fisi alisikiliza kwa makini majitapo ya ndovu. Aliamua kumpasulia ndovu mbarika: “Bwana ndovu najua kuwa wewe una nguvu na uwezo mkubwa wa kifedha.Lakini hayo yote mimi hayanihusu ni yako na familia yako. Sitakuruhusu unidhulumu kilicho haki yangu. Usiutumie uwezo uliopewa na Muumba kuwaonea na kuwanyanyasa maskini wasio mbele wala nyuma” alimaliza usemi wake na kuondoka huku machozi yakimdondoka.Fisi alipofika nyumbani, aliwasimulia fisi wanyongewenzake yaliyomsibu.Fisi walikusanyika na kulizingira boma la ndovu huku wakisema: “Tunataka haki itekelezwe! Dhuluma lazima ikome!

Unyanyasaji lazima ukome!” Ndovu aliposikia kelele langoni mwake, alipiga simu kwenye kituo cha polisi. Mara, kikosi cha polisi wa kupambana na ghasi kiliwasili. Fisi walipigwa mijeledi na kuezekwa marungu. Waliojifanya mabingwa walipigwa risasi. Fisi waliosalia walikimbilia makwao, huku wakichechemea kwa maumivu. Mpaka wa leo fisi wangali wanatembea kwa kuchechemea.

***Maswali***

a) Usimulizi huu ni wa aina gani? Toa sababu. (alama 4)

b) Eleza mtindo wa lugha uliotumika katika hadithi hii. (alama 4)

c) Eleza sifa za ndovu katika hadithi hii. (alama 5)

d) Fafanua jinsi kisa hiki kinavyodhihirisha methali: ‘Mwenye nguvu mpishe’ (alama 4)

e) Je, hadithi zina umuhimu gani katika jamii? (alama 3)

# GOLDLITE ONLINE SUPPLIES

***Hati ya kuhitimu kisomo cha sekondari kenya(kcse)***

# MITIHANI YA PAMOJA YA SHULE ZA KITAIFA 2025

**JINA: ……………………………………NAMBARI YA USAJILI: ………………………….**

**SAHIHI YA MTAHINIWA: ……………………TAREHE: ………………DARASA: …............**

**FASIHI: 102/3**

**KARATASI 3**

**MUDA: SAA 2½**

# MTIHANI WA PAMOJA WA LANJET

**KIDATO CHA NNE**

**MAAGIZO KWA WATAHINIWA**

***a)*** *Andika jina lako, shule na nambari ya mtihani kisha utie sahihi katika nafasi ulizoachiwa hapo juu.*

***b)*** *Jibu maswali manne pekee.*

***c)*** *Swali la kwanza ni la lazima.*

***d)*** *Maswali hayo mengine matatu yachaguliwe kutoka sehemu nne zilizobakiyaani Tamthilia,Riwaya,Hadithi Fupi na Fasihi Simulizi.*

***e)*** *Usijibu maswali mawili kutoka sehemu moja*

***f)*** *Majibu yote lazima yaandikwe kwa lugha ya Kiswahili pekee*

**KWA MATUMIZI YA MTAHINI PEKEE**

| Swali | Upeo | Alama |
|---|---|---|
| 1 | 20 | |
| | 20 | |
| | 20 | |
| | 20 | |
| JUMLA | 80 | |

CONTACT US ON:
WhatsApp/Call or Text 0724351706/0726960003
EMAIL: Goldlitepublishers@gmail.com

**SEHEMU YA A: USHAIRI** **(ALAMA 20)**

**1. LAZIMA**

Na ujenge nyumba yako, jingi jasho likuoshe,
Ufyeke, upime na uweke nguzo,
Kisha paa uweke na ukandike,
Siku nyingi bila kuingiliwa na mgeni hutakaa.

Wataanza kutalii mpaka mende usiku,
Nje na ndani ya  nyumba watazunguka,
Bila woga, bila ruhusa ulichonacho watakula,
Masalia yatakuwa yako, ijara ya kaziyo.

Na nyingi dawa uweke, nyumba nzima uihame,
Ukae nje nzima siku usubiri,
Wazima wamelala ukirudi usiku,
Vichwa vigumu hawafi mende rahisi.

Kifo cha mende sharti miguu juu
Kichwa ukikanyage kipasuke usikie,
Na kisha wengine usiku mchana uwasake.
Mpaka watakapokwisha.  Usiseme nao.

**Maswali**

**a)** Hili ni shairi la aina gani? (alama 1)

**b)** Eleza **muundo** wa shairi hili (alama 3)

**c)** Eleza jinsi mshairi alivyoutumia **uhuru** wake katika utunzi wa shairi hili. (alama 4)

**d)** Taja mbinu **mbili za lugha** alizotumia mshairi na uzitolee mifano. (alama 4)

**e)** Andika **ubeti wa tatu** kwa lugha nathari. (alama 4)

**f)** Eleza **ujumbe** wa mshairi. (alama 2)

**g)** Toa mfano mmoja wa mshororo **mshata**. (alama 1)

**h)** Kichwa gani kinaliafiki shairi hili? (alama 1)

## SEHEMU YA B:TAMTHILIA

## BEMBEA YA MAISHA (TIMOTHY M. AREGE)

***Jibu swali la 2 au 3***

**2.**‘’ Lakini ndiyo tabia yenu wanawake.Miaka inaposonga kama hivi mnatuona kama...kama…kama vile tambara bovu.’’

**a)** i)Yaweke maneno haya katika **muktadha** wake. (Alama 4 )

ii)Tambua mbinu **mbili** za kimtindo katika dondoo. (Alama 2)

**b)** Fafanua **umuhimu wa msemaji** katika kujenga ploti. (Alama 4)

**c)** **Utamanduni** huthaminiwa sana na jamii ya tamthilia ya Bembea ya Maisha. Jadili ukweli wa kauli hii kwa kutoa mifano **kumi** mwafaka tamthiliani. (alama 10)

**3.** Beni:Afadhali hao.Mjukuu wangu hatofautishi kondoo,mbuzi na mbwa.Wote hao kwake yeye ni mbwa!(*wanacheka wote)*

Yona: Inachekesha.

***Swali :*** Mazungumzo haya kati ya Beni na Yona yanabainisha tofauti iliopo kati ya suala la *usasa na ukale*. Kwa kutoa mifano **kumi** inayoonyesha usasa na **kumi** inayoonyesha ukale,linganua masuala haya. (alama 20)

## SEHEMU YA C: RIWAYA

## NGUU ZA JADI:*CLARA MOMANYI*

***Jibu swali la 4 au 5***

4.“Naweza kuoa wakati wowote na idadi yoyote ya wanawake.”

**a)** Weka dondoo hili katika **muktadha** wake. (alama 4)

**b)** Tambua **maudhui** katika dondoo hili. (alama 4)

**c)** Kwa kutoa mifano **kumi na miwili** mwafaka kutoka riwayani,onyesha jinsi maudhui uliyotambua hapo juu(4b) yalivyoshughulikiwa na mwandishi. (alama 12)

5. **Tamaa na ubinafsi** ni baadhi ya masuala makuu yaliyoshughulikiwa kwa mapana na marefu na *Clara Momanyi* katika riwaya yake ya *Nguu za Jadi*. Kwa kutoa mifano mwafaka riwayani thibitisha ukweli wa kauli hii. (alama 20)

## SEHEMU YA D :HADITHI FUPI

## MAPAMBAZUKO YA MACHWEONA HADITHI NYINGINE

***Jibu swali la 6 au 7***

**WINNIE NYARURI OGENCHE:SABINA**

**6.** *Maneno ya ripota huyo yalimwiingia Ombati maskioni yakasalia huko.Hayakufika akilini.Mwalimu mkuu alipenya kwenye umati uliokuwa umeanza kuwa mkubwa na kumtaka Ombati awaelekeze alikokuwa Sabina .Kabla ya Ombati kuwajibu,Sabina alifika nyumbani amevaa rinda kuukuu huku harufu ya samadi inamvuka.Watu waliokuwa wakimngoja walimzoa juujuu na kuanza kuimba tena. Ombati aliwafurusha wageni waliokuja kumwoa Sabina pamoja na mifugo wao.Baada ya kufanya hivyo,alijiunga na Sabina kuhojiwa na kupigwa picha.Alijitanua jinsi alivyotunukiwa kumlea mwana mwepesi masomoni.*

a)Eleza umuhimu wa mhusika Sabina katika **kukuza hadithi husika**. (alama 6)

b)Kwa kutoa mifano mwafaka kutoka kifunguni,onyesha **aina nne za taswira** zilizojitokeza. (alama 4)

c)Fafanua **changamoto** zinazokabili jinsia ya kike kwa mujibu wa hadithi hii. (alama 10)

**YUSSUF SHOKA HAMAD:** ***Mzimu wa Kipwerere***

**7.**"…*Kabla mwanamke yule hajakiwasha kile kibatari,nilijitokeza mle mvunguni na maguo yangu meupe kama ya maiti nikaangua mwangwi mkali mfano wa parapanda ya siku ya kiama."*

(a) Yaweke maneno haya katika muktadha wake. (Alama 4)

(b) Fafanua umuhimu wa mandhari katika dondoo hili. (Alama 4)

(c) Fafanua mbinu za kimtindo katika dondoo hili. (Alama 2)

(d) Onyesha jinsi itikadi ilivyomwezesha *mlinda mzimu na wahenga waliotukuka* kuwafanya wanakijiji kuogopa na kuamini mzimu wa Kipwerere kiasi cha kutofanya mzaha na maeneo yale ambayo mzimu uliotea.. (alama 10)

## SEHEMU YA E: FASI HI SIMULIZI

***Swali la nane***

8. a) Ulumbi ni nini? (alama 2)

ii) Ulumbi hutekeleza **majukumu** gani katika jamii?. ( alama 6)

iii) Eleza **vipengele sita** vya kuzingatia katika uchanganuzi wa hadithi. (alama 6)

b) Eleza namna ambavyo hadhira huhusishwa katika uwasilishaji wa fasihi simulizi. ( alama 6)

CONTACT US ON:
WhatsApp/Call or Text 0724351706/0726960003
EMAIL: Goldlitepublishers@gmail.com

GOLDLITE ONLINE SUPPLIES
MTIHANI WA PAMOJA WA SHULE ZA KITAIFA
*Hati ya kuhitimu kisomo cha sekondari*

# 102/3 - KISWAHILI - (Fasihi)

**Jina ………………………………………………..……… Nambari………………………………………**

**Sahihi ………………….…...………………….............Tarehe……………………………………......**

# SHULE YA UPILI YA MANGU

**Maagizo**

a) *Andika Jina lako na nambari yako ya mtihani katika nafasi ulizoachiwa hapo juu*
b) *Tia sahihi yako kisha uandike tarehe ya mtihani katika nafasi ulizoachiwa hapo juu*
c) *Jibu maswali* ***manne*** *pekee*
d) *Swali la* ***kwanza*** *ni la* ***lazima***
e) *Maswali hayo mengine matatu yachaguliwa kutoka sehemu nne zilizobaki, yaani: Riwaya, Tamthilia, Fasihi simulizi na Hadithi Fupi*
f) *Usijibu maswali* ***mawili*** *kutoka* ***sehemu moja***
g) *Majibu yote* ***lazima*** *yaandikwe kwa lugha ya Kiswahili*

Watahiniwa ni lazima wahakikishe kwamba kurasa zote za karatasi hii zimepigwa chapa sawasawa na kuwa maswali yote yamo.

## SEHEMU A: USHAIRI

**Swali la lazima.**

1.**Soma shairi lifuatalo kisha ujibu maswali.** (alama 20)

Mbio hizino twendazo, twendapi mbio hizino?
Mbio zisizo viuzo, ni mbio za mashindano!
Mbio za mfululizo, mbele zina mgongano
Mbio hazina vigezo, twaendapi mwendo huno?

Mbio zina matatizo, pasipo maelewamo
Mbio kwenye mtelezo, watu hugwa na miguno
Mbio hazileti tuzo, mbona huu mwandamano
Mbio ni njia ambazo, twenende mwendo mnono.

Mbio nguo uvaazo, hufichi hata kiuno
Mbio jicho mlegezo, ajaye ni tangamano
Mbio chini kwa mlazo, huogopi kisonono?
Mbio watoa pumbazo, kila rijali ni vuno.

Mbio hazino mchezo, huhitaji mshikano
Mbio zenye mwelekezo, zendwazo kwa maagano
Mbio ziwe mjalizo, hatua kwa mfwatano
Mbio siwe mfukuzo, ukenda mwendo wa sono.

Mbio bora zifaazo, sizo za mafarakano
Mbio tena kwa tangazo, tuanze sawa pambano
Mbio si kwenye pambizo, sote ndani mfwatano
Mbio si maangamizo, mwendo ukawa mbano.

Mbio si nyimbo zimbwazo, midomoni kwa maneno
Mbio ni sera ambazo, mepangwa kwa mlingano
Mbio ziwe mageuzo, maisha yawe manono
Mbio si mlimbikizo, ni uchoyo mwendo huno.

Mbio rijali mwendazo, kila saa mchuwano
Mbio banati si hizo, kuridhi haja za ngono
Mbio dada uigazo, usilingane na pono
Mbio huweki vikwazo, mwendo utakata kano.

Mbio kwao hamnazo, musosikia maneno
Mbio mali mzo mzo, zilizo mrundikano
Mbio wachache wanazo, wengi wana misinono
Mbio bora ni chagizo, mwendo uso na mibano.

Mbio zangu maagizo, kwa weledi wa maneno
Mbio zenye mahimizo, kuleta utangamano
Mbio za maendelezo, sare bila utengano
Mbio si za mchuchuzo, mwendo uso na mfano.

**Maswali.**

(a) Eleza aina ya ushairi huu. (alama 1)

(b) Shairi hili linaangazia nyendo ainati. Thibitisha nyendo hizi kwa kutoa mifano **sita** kutoka kwenye shairi. (alama 3)

(c) Fafanua umuhimu wa aina mbili za urudiaji zilizotumiwa katika shairi hili. (alama 3)

(d) Bainisha nafsineni katika shairi hili. (alama 2)

(e) Eleza kwa kutoa mfano, mbinu mbili ambazo mshairi ametumia kutosheleza mahitaji ya kiarudhi. (alama 3)

(f) Shairi hili ni la mkondo gani? Thibitisha. (alama 2)

(g) Eleza toni ya mshairi. (alama 1)

(h) Eleza umuhimu wa maswali ya balagha yaliyotumika. (alama 2)

(i) Eleza ujumbe unaojitokeza katika ubeti wa mwisho. (alama 2)

(j) Eleza msamiati wa maneno yafuatayo kama yalivyotumiwa katika ushairi. (alama 1)

(i) Rijali

(ii) Mbano

**SEHEMU B:**

## SEHEMU C. TAMTHILIA

**T. Arege: Bembea ya Maisha**

**Jibu swali la 4 au la 5**

4."... wakati mwingine mwindaji huwa mwindwa. Hata kijijini wanaishi watu . Watu hao hawakumbwi na dhiki kiasi hiki. Ya nini kung'ang'ana kuyatafuta maisha kama kwamba hayapiti? Maisha ni mshumaa uso mkesha! Ukijiachia sana peupe hata upepo unaweza kuuzima kabla ya kulika hadi nchani."

**Maswali**

a) Eleza muktadha wa dondoo hili. (alama. 4)

b) Bainisha toni katika kauli hili (alama. 2)

c) Eleza vipengele **vinne** vya kimtindo alivyotumia msemaji kufanikisha uwasilishaji wa ujumbe. (alama. 4)

d) Eleza umuhimu wa msemaji katika kuendeleza ploti ya tamthilia hii. (alama 10)

***au***

5. (a) Fafanua umuhimu wa mazungumzo kati ya Luka, Beni na Yona katika kujenga tamthilia ya "Bembea ya Maisha" (alama 10)

(b) "Bembea inapolika na kukatika haiwi mwisho wa michezo.Huungwa na mchezo kuanza tena." Thibitisha ukweli wa kauli hii kwa kutolea mifano mwafaka tamthiliani. (alama. 10)

**SEHEMU YA D: HADITHI FUPI: MAPAMBAZUKO YA MACHWEO NA HADITHI NYINGINE.**

1. "Yu wapi kirukanjia wako? Wajua yuko wapi? Uliacha mbachao kwa msala upitao. Atakutunza nani, maana kwako fadhila za punda ni mashuzi!"

a. Yaweke maneno haya katika muktadha wake. (alama 4)

b. Taja mbinu mbili za lugha zilizotumika katika dondoo hili. (alama 2)

c. Bainisha toni ya dondoo. (alama 1)

d. Fafanua sifa zozote tatu za mzungumziwa. (alama 3)

e. Kwa kurejelea hadithi "Fadhila za punda" onyesha ukweli wa kauli kuwa fadhila za punda ni mashuzi kwa mifano mwafaka. (alama 10)

**Au**

2. Huku ukirejelea hadithi zifuatazo tano jadili maudhui ya migogoro kwa kutoa mifano maridhawa. (alama 20)
    a. Fadhila za punda
    b. Msiba wa kujitakia
    c. Mapambazuko ya machweo
    d. Harubu ya maisha

**SEHEMU E : FASIHI SIMULIZI**

**8.** **a)** Miviga ni nini ? (alama 2)

**b)** Fafanua sifa zozote sita za miviga. (alama 12)

**c)** Miviga ina majukumu yapi katika jamii ? (alama 6)

# GOLDLITE ONLINE SUPPLIES

*Cheti cha Kuhitimu Kisomo cha Sekondari*

## TATHMINI YA MAJARIBIO (I), 2025

**102/3 Kiswahili - Fasihi Karatasi ya 3**

**KIDATO CHA NNE 2025 Saa: 2½**

***MOI KAMUSINGA.MARANDA.CARDINAL.KIBABII.KEVEYE.MUSINGU***

**Jina: ……………………………………Nambari: …………..Tarehe…….................**

**Mkondo:………… Shule:..................................................Sahihi:………..................**

**Maagizo**

a) ***Andika jina lako, nambari ya usajili, mkondo, sahihi na tarehe katika nafasi ulizoachiwa hapo juu.***
b) ***Jibu maswali manne pekee.***
c) ***Swali la kwanza ni la lazima.***
d) ***Maswali hayo mengine matatu yachaguliwe kutoka sehemu nne zilizobaki; Riwaya, Hadithi Fupi, Ushairi na Fasihi simulizi***
e) ***Usijibu maswali mawili kutoka sehemu moja.***
f) ***Karatasi hii ina kurasa 18. Watahiniwa ni lazima wahakikishe kwamba kurasa zote za karatasi hii zimepigwa chapa sawasawa na kuwa maswali yote yamo.***

**Kwa matumizi ya mtahini pekee**

| SWALI | UPEO | ALAMA |
|---|---|---|
| 1 | 20 | |
| | 20 | |
| | 20 | |
| | 20 | |
| JUMLA | 80 | |

**CONTACT US ON:**
**WhatsApp/Call or Text 0724351706/0726960003**
**EMAIL: Goldlitepublishers@gmail.com**

## SEHEMU A: TAMTHILIA

**Timothy Arege: *Bembea ya Maisha***

**1.** Lazima

" Umesahau kuwa mimi ni mume. Mimi ni kichwa na kwamba wewe ni shingo. Ninaona ushakata ubeleko unasubiri siku ya siku."

a) Weka dondoo hili katika muktadha wake (alama 4)
b) Tambua toni inayojitokeza katika dondoo hili. (alama 2)
c) Jadili umuhimu wa msemewa wa maneno haya katika kufanikisha ploti kwenye tamthilia *Bembea ya Maisha.* (alama 4)
d) Tathmini mchango wa mila na tamaduni katika kudidimiza maendeleo katika jumuiya ya *Bembea ya Maisha*. (alama 10)

## SEHEMU B: RIWAYA

**Clara Momanyi: *Nguu za Jadi***

***Jibu swali la 2 au 3***

**2.** "Sheria kali za nchi zilipitishwa kuhusu mihadarati. Sumu hizo zilikuwa tisho kwa usalama na ustawi wa nchi. Lakini sheria hizi ziliishia kwenye mabuku ya serikali. Biashara hiyo ikazidi kunoga. Vijana wengi wakawa wanapoteza maisha yao ... aliwekea fedha alizovuna katika biashara hiyo haramu kwenye majumba ya starehe na anasa. Alikuwa na vilabu vingi vilivyotapakaa mjini. Katika vilabu hivi, biashara za kila aina zilinoga. Vilabu vingine viliwameza vigoli wa mji usiku na kuwatapika asubuhi.

a) Changanua mbinu za kimtindo katika dondoo hili. (alama 6)
b) Eleza athari za ufisadi kwa kurejelewa jumuiya ya *Nguu za Jadi*. (alama 14)

**3.** "Ndugu zangu, lazima tupiganie kilicho chetu. Lazima tujifunze kusema hapana. Asiyeweza kusema hivyo, bila shaka atakuwa fukara maishani. Msikubali kwenda popote mtakapoelekezwa. Matango ndiyo makao yenu, na ndipo mtakapoishi... "

a) Eleza muktadha wa dondoo hili (alama 4)
b) Msemaji wa maneno haya ni mwanamapinduzi. Thibitisha kwa hoja nne kwa kurejelea riwaya *Nguu za jadi.* (alama 4)
c) Eleza mikakati anayochukua msemaji na wanamatuo wenzake kupigania haki zao kwa kurejelea riwaya ya *Nguu za Jadi* (alama 12)

## SEHEMU C: HADITHI FUPI

**D.W Lutomia na Phibian Muthama (Wahariri): *Mapambazuko ya Machweo na Hadithi Nyingine***

***Jibu swali la 4 au la 5.***

**CONTACT US ON:**
**WhatsApp/Call or Text 0724351706/0726960003**
**EMAIL: Goldlitepublishers@gmail.com**

**Yussuf Shoka Hamad: *Mzimu wa Kipwerere***

**4.** a) "Nisamehe mwanangu, nisitiri mwanangu, nizike duniani unifunike akhera, mwanangu! Ni kweli yote uliyoyasema lakini ujue tu kama siko peke yangu."

i. Msemaji wa kauli hii ana hulka kinzani. Thibitisha. (alama 6)

ii. "Uchaji wa mandhari ambamo mazungumzo haya yamejikita ni kichocheo kikuu cha makuruhu ya binadamu." Hakiki ukweli wa kauli hii, kwa hoja saba ukirejelea hadithi *Mzimu wa Kipwerere*. (alama 7)

**Winnie Nyaruri Ogenche: *Sabina***

b) Mizizi ya elimu ni michungu ila matunda yake ni matamu. Thibitisha ukweli wa kauli hii ukirejelea hadithi ya *Sabina*. (alama 7)

**5.** a) Fafanua mikakati inayochukuliwa na wanawake kukabiliana na changamoto zinazowakumba ukirejelea hadithi zifuatazo:

i. *Nipe Nafasi* (alama 6)

ii. *Fadhila za Punda* (alama 6)

**Dominic Maina Oigo: *Kifo cha Suluhu***

b) Jadili umuhimu wa barua ya Bi. Suluhu kwa Suluhu katika kufanikisha anwani ya hadithi *Kifo cha Suluhu*. (alama 8)

## SEHEMU E: USHAIRI

***Jibu swali la 6 au la 7.***

**6.** *Soma shairi lifuatalo kisha ujibu maswali:*

Binadamu hatosheki, ni kiumbe chenye zani, kweli mja hapendeki,
Kwa kweli haaminiki, hila ameficha ndani, la wazi ni unafiki
Ukweliwe haafiki, njama zake zi moyoni, usimwone ni rafiki
Mtu kuwa na tamaa, akitaka kiso chake, ni hatari kama nyoka,

Wengine watakuua, wakiona una pesa, hata zikiwa kidogo,
Hizo kwao ni maua, hupupiwa zikatesa, wakazifuata nyago,
Hadi kwenye wako ua, pasipo hata kupesa, wala kukupa kisogo,
Mtu kuwa na tamaa, akitaka kiso chake, ni hatari kama nyoka

Pindi kinunua kitu, hafurahi Shaitani, bali tajawa chukizo,
Mtu kiwa mtukutu, tanuna mtimani, kwalo lako tekelezo,
Tamko lake 'Subutu' Kuondoa tumaini, na kukuulia wazo,

Mtu kuwa na tamaa, akitaka kiso chake, ni hatari kama nyoka,

Aliye na taraghani, taabu kuishi naye, kazi yake kujidai,
Takusema faraghani, asosema kiwa naye, kupendeza maadui,
Hana faida nyumbani,ni mtu akuchimbaye, mradi usitumai,
Mtu kuwa na tamaa, akitaka kiso chake, ni hatari kama nyoka,

Kwa hakika ni balaa, kumkirimu mchawi, aliyejaa uchoyo,
Bahati ina hadaa, kukupa alo sadawi, aibatili rohoyo,
Mipangoyo kwake jaa, na nia ya ustawi, huwiza kuvunja kaninyo,
Mtu kuwa na tamaa, akitaka kiso chake, ni hatari kama nyoka.

Ninacho changu kilio, ninalia sanasana, kinyesi nimetupiwa,
Ningetoa azimio, lakini uwezo sina, kwa matatizo kuambiwa,
Ama nitumie mbio, fuadini ninanena, akilini nazuiwa,
Mtu kuwa na tamaa, akitaka kiso chake, ni hatari kama nyoka.

*(kutoka kwa malenga wa ziwani)*

*Maswali*

a) Fafanua mambo saba ambayo nafsineni analalamikia. (alama 7)

b) Ainisha shairi hili kwa kuzingatia vigezo vifuatavyo: (alama 3)
   i. Idadi ya vipande katika kila mshororo.
   ii. Mpangilio wa vina katika kila ubeti.
   iii. Idadi ya mishororo katika kila ubeti.

c) Andika ubeti wa nne katika lugha tutumbi (alama 4)

d) Bainishaumuhimu wa tamathali mbili za usemi zilizotumiwa katika shairi hili (alama 4)

e) Andika aina mbili za urudiaji zilizotumiwa katika shairi hili (alama 2)

**7. *Soma shairi lifuatalo kisha ujibu maswali***

Ndugu Makanyaga nakutambia
Hii fupi hadithi
Kuhusu yaliyojiri kwetu kijijini.
Ulipokuwa wewe mlinzi kijijini.

Ndugu Makanyaga, yule mbuzi
Sasa naona ana mwenyewe
Baada ya kiamboni wewe kinara kumtoa
Dhambi za kijiji abebe
Mwituni ukamfunga kwa kigingi hafifu
Kusudi baharini azame
Au mwituni kupotelea
Aliwe na wanyama

Mradi umejikosha

Lakini ndugu Makanyaga,
Tangu lini mbuzi kutakasa kijiji?
Hujui ni lazima mwanadamu kujirudi?
Na msamaha kuomba?

Ndugu Makanyaga!
Mbuyu hauangushwi kwa upanga!
Kutumia wembe ni sanamu tosha
Halaiki kualika kushuhudia
Sinema ya bure kijijini.

Kama huamini waulize Wareno, watakujuza:
Mbao na mawe ni vitu mbalimbali
Mshabaha vimekosa tangu hapo
Ndo maana, mpaka leo imesimama.

Ndugu Makanyaga, mbwa mkali ni ngao ya mji
Mbwa hatiwi kitanzi kwa genge kufokea
Hakuna atakaye jina kubwa
Ambalo mkia hukunja kwa mbisho wa jizi.

Ndugu Makanyaga!
Yule mbwa ulomuua
Sauti yake inadai haki
Na yule mbuzi ulomhini
Mwenyewe amepata wa kumtunza.

Ndugu Makanyaga, umeteleza!

Nami sasa ndugu nakujuza
Dambi za mwanadamu hazisafishwi tena
Kwa damu ya mwanakondoo
Ni lazima kijiji kuubeba wake mzigo
Kijiji hakitatakasika kwa kutoa kafara
Lazima kwanza mioyo itakasike;
Nyoyo dhaifu za waja!

Timothy Arege*: Tunu ya Ushairi*

<u>*Maswali*</u>

**CONTACT US ON:**
**WhatsApp/Call or Text 0724351706/0726960003**
**EMAIL: Goldlitepublishers@gmail.com**

a) Onyesha jinsi mwandishi alivyotumia mbinu zifuatazo kufanikisha maudhui kwenye shairi hili:
   i. Aina za taswira (alama 4)
   ii. Kinaya (alama 2)
b) Mtunzi wa shairi hili amekiuka kanuni za arudhi kwenye shairi hili. Thibitisha kwa hoja nne. (alama 4)
c) Tambua toni inayojitokeza katika ubeti wa mwisho wa shairi hili. (alama 2)
d) Toa mfano wa na uonyeshe dhima tatu za mishata katika shairi hili. (alama 4)
e) Andika ubeti wa pili kwa lugha nathari. (alama 4)

## SEHEMU E: FASIHI SIMULIZI

**8.** *Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali*

a) Nina vitu vitatu: kuku, nguchiro na mtama. Nimefika mtoni nami nataka nivivushe vitu hivi. Mashua yangu ina uwezo wa kunivusha mimi na kitu kimoja tu. Vyote lazima vivushwe. Siwezi kumwacha nguchiro na kuku kwa sababu nguchiro atamla kuku. Naye kuku akiachwa pamoja na mtama ataula. Nitafanyaje?
   i. Tambua kipera cha utungo uliopewa. Thibitisha. (alama 3)
   ii. Taja jibu la kifungu hiki. (alama 1)
   iii. Tambua sifa za kimuundo zinazojitokeza kwenye kifungu. (alama 2)
b) Eleza umuhimu wa kutumia mbinu ya kushiriki wakati wa uwasilishaji wa fasihi simulizi. (alama 5)
c) Fafanua sababu nne za kufaragua katika fasihi simulizi. (alama 4)
d) Wimbo wa taifa huwa chini ya utanzu wa nudhuma. Fafanua njia tano zinazoweza kutumiwa kuboresha uwasilishaji wake kwenye gwaride la shule yako. (alama 5)

**CONTACT US ON:**
**WhatsApp/Call or Text 0724351706/0726960003**
**EMAIL: Goldlitepublishers@gmail.com**

# GOLDLITE ONLINE SUPPLIES

***Hati ya kuhitimu kisomo cha sekondari kenya(kcse)***

# MITIHANI YA PAMOJA YA SHULE ZA KITAIFA 2025

**JINA: ………………………………………NAMBARI YA USAJILI: …………………………….**

**SAHIHI YA MTAHINIWA: ……………………TAREHE: ………………DARASA: …............**

# SHULE YA UPILI YA MASENO

**102/3 FASIHI**

**KARATASI YA TATU**

**MUDA:2:30**

**MAAGIZO**

*a) Jibu maswali manne pekee*

*b) Swali la kwanza ni la lazima.*

*c) Maswali mengine matatu yachaguliwe kutoka sehemu tatu zilizobaki*

*d) Usijibu maswali mawili kutoka sehemu moja*

*e) Kila swali ni alama 20*

*f) Majibu yote yaandikwe kwa lugha ya Kiswahili.*

**KWA MATUMIZI YA MTAHINI**

| SEHEMU | UPEO | ALAMA |
|---|---|---|
| A:RIWAYA | 20 | |
| B:TAMTHILIA | 20 | |
| C:HADITHI FUPI | 20 | |
| D:USHAIRI | 20 | |
| E:FASIHI SIMULIZI | 20 | |
| JUMLA | 80 | |

**SEHEMU A: RIWAYA:NGUU ZA JADI na Clara Momanyi**

CONTACT US ON:
WhatsApp/Call or Text 0724351706/0726960003
EMAIL: Goldlitepublishers@gmail.com

## SWALI LA LAZIMA

## SEHEMU A:RIWAYA :NGUU ZA JADI na Clara Momanyi

**1.** "…………………*Tubadilishe mielekeo ya fikra zetu zilizotiwa usugu na kudumazwa na hisia za kikabila. Ndugu zangu, ukabila ni sumu ya nyoka*

A. Weka dondoo hili katika muktadha wake (al 4)

B. Fafanua umuhimu wa msemaji kwa kurejelea riwaya nzima (al 4)

C. Eleza mbinu mbili za kimtindo zilizotumiwa kwenye dondoo hili (al 2)

D. Eleza jinsi mwandishi wa Nguu za Jadi alivyosawiri maudhui ya mapuuza (al 10)

## SEHEMU B:TAMTHILIA :BEMBEA YA MAISHA na Timothy Arege

**Jibu swali la 2 au la 3**

2) "Eti hajakosa adabu? Mtu ana ubaguzi kama nini! Ana moyo mgumu kama jiwe! Amejaliwa lakini bahili kama mchanga wa dhahabu. Hajui mali ya bahili huliwa na wadudu?

a) Eleza muktadha wa dondoo hili.(al.4)

b) Tathmini umuhimu wa maswali ya balagha katika dondoo hili.(al.2)

c) Bainisha na kutoa mifano vipengele vingine viwili vya kimtindo katika dondoo hili.(al.4)

d) Fafanua nafasi ya anayeitwa bahili katika dondoo hili katika kuijenga tamthilia ya Bembea ya Maisha .(al.10)

**au**

3) a) Jadili namna tamthilia ya Bembea ya Maisha inavyoshughulikia suala la elimu.(alama 8)

b) Eleza umuhimu wa mazungumzo baina ya Luka, Yona na Beni katika kukuza vipengele hivi vya fasihi:

i) Maudhui ( alama 8)

ii) Wahusika (alama 4)

## SEHEMU C:HADITHI FUPI:Mapambazuko ya Machweo na Hadithi nyingine

**J**ibu swali la 4 au la 5

4."Thankyou. U mteja wa kipekee, unajua kuthamini huduma nzuri unapopewa. Kwaheri ya kuonana. Natumai tutakutana hivi karibuni."

a) Eleza muktadha wa dondoo hili (al 4)

b) Eleza masaibu yaliyompata msemewa wa dondoo hili (al 16)

CONTACT US ON:
WhatsApp/Call or Text 0724351706/0726960003
EMAIL: Goldlitepublishers@gmail.com

Au

5.Ukombozi wa wanawake umekumbwa na vizingiti vingi. Jadili ukweli wa kauli hii kwa kurejelea hadithi:

Sabina (alama 10)

Nipe nafasi (alama 10)

**SEHEMU D:USHAIRI**

**Jibu swali la 6 au 7**

6.Soma shairi lifuatalo kisha ujibu maswali yanayofuata.

Msitu nikakuta, nyuki wamo mzingani
Kwa juhudi wanakita, mara nje mara ndani
Husuda wameikata, hata hawasengenyani
Nyuki ni wadudu duni, wanashinda kwa umoja

Mchwa nao nikaona, wamejenga maskani
Waanya bidii sana, uvivu hawatamani
Wao husaidiana, tena hawadanganyani
Mchwa wadudu wa chini, wanaishi kwa umoja

Nalo jeshi la siau, hutandawaa njiani
Laenda bila ya hofu, maana ajiamini
Silaha zao dhaifu, meno tena hawaoni
Wa kuwatadia nini?Kwani wanao umoja

Nao chungu wachukuzi, nyama warima njiani
Masikini wapagazi, mizigo yao kichwani
Ingawa si wachokozi, wakali ukiwahini

Katu hawafarakani, wanadamu kwa umoja

Sisi ni wana Adamu, mbona hatusikizani,
Tusitietie hamu, ukubwa kuutamani
Wachache wataalamu, tuwasadi kwa imani
Hii "Huyu awezani," yatuvunjia umoja

**Maswali**

a) Fafanua kikamilifu dhamira katika shairi hili. (alama 1)
b) Ni sifa zipi nne zinazopewa wanaozungumziwa? (Alama 4)
c) Onyesha insi mwandishi alivyotumia uhuru wakw katika shairi hili. (Alama 2)
d) Ainisha shairi hili kutegemea: ( Alama 4)
    i) Idadi ya mishororo katika ubeti
    ii) Idadi ya vipande katika mshororo
    iii) Mpangilio wa vina
    iv) Mshororo wa mwisho katika beti
e) Andika ubeti wa mwisho kwa lugha tutumbi. (Alama 4)
f) Eleza toni katika shairi hili.( Alama 2)
g) Eleza nafsi-neni katika shairi hili. (Alama 1)
h) Fafanua maana ya maneno yafuatayo kama yalivyotumika katika shairi hili. (Alama 2)
    Chungu
    Tuwasadi

Au

7.Wingu jeusi latoka, kusi hadi kaskazi,
Mashariki ladondoka, magharibi si ajizi,
Mno tuna shakashaka, twapata ja sisimizi,
Kuteleza siku hizi, hakika ni kuanguka.

Roho zinatilifika, kuwahiliki mahiri,

Wanaochovya gharika, starehe ya dahari,
Kina cha mto kumbuka, ki tuli kikiri,
Siku hizi kuteleza, hakika ni kuanguka.

Ukidhubutu wazama, muda wa toba hupati,
Ukichovya ni nakama, kalima iwe laiti,
Na yetu bure huruma, waama ni tashtiti,
Siku hizi kuteleza, hakika ni kuanguka.

Hutelezi ukaima, naamba wazi sifumbi,
Pulika haiwi homa, ungawa nao ujimbi,
Sambe mzizi hatoma, nyendoze zina mlimbi,
Siku hizi kuteleza, hakika ni kuanguka.

Nafaka ashasumisha, dungudungu simuoni,
Majibwa anagurisha, hawanusuriki nyani,
Ya mbwa chunga maisha, nyani kaidi ta'bani,
Siku hizi kuteleza, hakika ni kuanguka.

Kokote kuna maua, ela mengi yana sumu,
Yosayosa yanaua, anayenusa hadumu,
Bora jangwa kutengewa, kuepuka chungu tamu,
Siku hizi kuteleza, hakika ni kuanguka.

Hamna kamwe shufaka, hupati wala shufaa,
Hatima ya kuteguka, tiketi kuangamia,
Mzuri wa kupulika, afaa kuchanjamaa,
Siku hizi kuteleza, hakika ni kuanguka.

CONTACT US ON:
WhatsApp/Call or Text 0724351706/0726960003
EMAIL: Goldlitepublishers@gmail.com

a. Eleza dhamira ya shairi hili. (al.2)

b. Fafanua ujumbe wa shairi hili ukizingatia ubeti wa kwanza hadi

wa tano. (al.3)

c. Tambua njia mbili anazotumia mshairi kuusisitiza ujumbe wake.(al.2)

d. Bainisha matumizi ya vipengele vifuatavyo katika utungo huu. (al. 3)

i. Usimulizi

ii. Tasfida

iii.Tanakuzi

e) Tambua hadhira lengwa katika shairi hili.(al.1)

f) Fafanua toni ya shairi hili.(al.1)

g) Ainisha shairi hili kwa bahari mbili na utoe sababu.(al.2)

h) Eleza mbinu mbili ambazo mtunzi ametumia kutoshelesha mahitaji ya kiarudhi.(al.2)

i) Andika ubeti wa sita kwa lugha nathari.(al.4)

**SEHEMU E:FASIHI SIMULIZI**

**Jibu swali la 8**

8. a) Eleza faida tatu na hasara mbili za mbinu ya kurekodi katika kukusanya data ya vipera vya fasihi simulizi. (Alama 5)

b) Eleza tofauti tano kati ya fasihi andishi na fasihi simulizi.( Alama 5)

c) Soma kifungu hiki kisha ujibu maswali yanayofuata.

Punda wangu mbeba mizigo,

Ubebapo mizigo,

Wenzako hukutamani,

Kwa nguvu zako za ndovu,

Msimu wa mavuno waja,

CONTACT US ON:
WhatsApp/Call or Text 0724351706/0726960003
EMAIL: Goldlitepublishers@gmail.com

Ulitima kuniondolea,

Punda wangu kipenzi cha wateja wangu,

Ulianza kubeba kilo hamsini,

Sasa wabeba dunia nzima

Wazee wazangu wananionea gere

Kwa ubora wako

Wakwe wamenishauri, kukutuza wao kama mahari.

We! Punda wangu, sikupeani ng’o!

a) Thibitisha kuwa hiki ni kipera cha tondozi. (Alama 2)

b) Bainisha vipengele vitatu vya kimtindo katika kiungu hiki. (Alama 3)

**c)** Kipera hiki cha tondozi kimeanza kufifia katika jamii yako. Eleza mikakati mitano unayoweza kuitumia kuhakikisha hakijapotea. (Alama 5)

# GOLDLITE ONLINE SUPPLIES

***Hati ya kuhitimu kisomo cha sekondari kenya(kcse)***

# MITIHANI YA PAMOJA YA SHULE ZA KITAIFA 2025

**Jina:………………………………………………………..……….Nambari:………………..…………**

**Sahihi ya Mtahiniwa:……………………….. Tarehe:…………..…………..2025**

# MTIHANI WA PAMOJA WA MERU

**102/3**

**KISWAHILI**

**KARATASI YA PILI**

**Maagizo**

*a)* Jibu maswali manne pekee.
*b)* Swali la kwanza ni la lazima.
*c)* Maswali hayo mengine matatu yachaguliwe kutoka sehemu nne zilizobaki yaani: Riwaya, Ushairi, Hadithi fupi na fasihi simulizi.
*d)* Usijibu maswali mawili kutoka sehemu moja.
*e)* Majibu yote lazima yaandikwe kwa lugha ya Kiswahili.
*f)* Majibu yote sharti yaandikwe kwenye kijitabu cha majibu ulichopewa.
*g)* Karatasi hii ina kurasa 15 zilizopigwa chapa.
*h)* Watahiniwa ni lazima wahakikishe kwamba kurasa zote za karatasi hii zimepigwa chapa sawasawa na kuwa maswali yote yamo.
***i)*** Andika nambari ya maswali uliyoyajibu kwenye jedwali ulilochorewa hapo chini.

**Kwa matumizi ya mtahini pekee**

| Swali | Upeo | Alama |
|---|---|---|
| | 20 | |
| | 20 | |
| | 20 | |
| | 20 | |
| Jumla | 80 | |

## SEHEMU A: HADITHI FUPI (LAZIMA)

*D.W. Lutomia na Phibbian Muthama* **: Mapambazuko Ya Machweo Na Hadithi Nyingine**

1. **Lazima**

Athari ya mawazo yake ilijiandika dhahiri shahiri usoni mwake. Alianza kwa kuachia tabasamu pana mithili ya msafiri aliyefika salama. Baada ya dakika chache, machozi yalianza kumtoka njia mbilimbili huku kajishika tama. Alifikiria kuhusu mtihani uliodhamiriwa kuanza siku ya Jumanne. Mtihani ambao ungemwezesha kupata ufadhili katika shule ya upili ya bweni ikiwa angepita vyema. Hili ndilo wazo lililozua tabasamu. Lakini, angefeli je? Hatima yake ingekuwa ipi? Maswali haya yalimliza yakamwacha akisinasina kama mgonjwa wa mafua. Akiwa katika hali hii, aliyakumbuka maneno ya mwalimu mkuu, "Mizizi ya elimu ni michungu ila matunda yake ni matarnu. Ikiwa mnataka kuyaonja matunda ya elimu, lazima mtie bidii kwani mtaka cha mvunguni sharti ainame." Akiwa amezama kwenye lindi la mawazo, alizinduliwa na sauti ya Yunuke ikimwita, "Sabina! Sabina! Sabinaa!"

***(a)*** Changanua mtindo kwenye kifungu. (alama 8)

***(b)*** Suala la kazi na bidi limeangaziwa kwa kina kwenye diwani ya mapambazuko ya machweo. Tetea ukweli wa kauli hii kwa kurejelea hadithi zifuatazo:

***i)*** Fadhila za punda

***ii)*** Mapambazuko ya machweo

***iii)*** Sabina (alama 12)

## SEHEMU B: RIWAYA

**Nguu za Jadi,** *Clara Momanyi*

*Jjibu swali la 2 au 3*

2. *"Ndege mliolelewa kizimbani nyie hamwezi kuruka. Mtawezaje ilihali mnaishi kufikiria kwamba kuruka ni ugonjwa.*

a) Eleza muktadha wa dondoo hili. (al.4)

b) Tambua mbinu ya uandishi atika dondoo hili. (al.2)

c) Fafanua matumizi mengine ya mbinu hii kwa kurejelea riwaya nzima. (al.14)

3 *"Wawekezaji wengi wamehamia nchi jirani kutokana na ufisadi uliokithiri katika jamii yetu. Sera za kufukarisha zinaendelea kuwanyanyasa wengi."*

a) Fafanua muktadha wa dondoo hili. (al.4)

b) Tambua maudhui katika dondoo hili. (al. 10)

c) Eleza sifa nne za msemaji wa maneno haya. (al.6)

## SEHEMU C: TAMTHILIA

**Timothy Arege:** Bembea Ya Maisha

Jibu swali la 4 au la 5

4. *"Hata nikiitwa nitaondoka nikiwa nimeridhika."*
   - ***a)*** Eleza muktadha wa dondoo hili . (alama 4)
   - ***b)*** Kwa hoja **tano**, eleza sifa za msemaji wa maneno haya . (alama 5)
   - ***c)*** Tambua mbinu **moja** ya lugha iliyotumika katika dondoo hili. (alama 1)
   - ***d)*** Wahusika mbalimbali kwenye tamthilia wamekubwa **na majonzi na furaha**. Thibitisha. (alama 10)

5. *"...Tayari unakuwa umeonja seli.Hata wahudumu wenyewe hawana mlahaka mwema .amri na vitisho kama askari.Unashindwa kama uuguze moyo ama ugonjwa.Katika wodi hewa iliyojaaa harufu ya dawa imezagaa,vitanda vimesalimu amri mpaka shiti zikagura.Yaani hali nzima haikupi matumaini ya kutoka ukiwa bora.matumaini yanadidimia .Tumaini lako unaliweka katika sala. "*

   (a) Tambua toni mbili katika kifungu hiki (alama 2)

   (b) Tambua aina mbili za taswira katika dondoo hili (alama 2)

   (c)Kando na taswira chambua vipengele vingine vya kimtindo (alama 6)

   (d) Fafanua namna mandhari ya dondoo hili yalivyochangia kujenga tamthilia ya Bembea ya Maisha. (alama 10)

## SEHEMU D: USHAIRI.

*Jibu swali la 6 au la 7*

6. Soma shairi lifuatalo kisha ujibu maswali

**<u>Taifa ni Ushuru</u>**

Lau kama ingakuwa, madhali tuna uhuru
Watu kodi kutotowa, na kuifanya kufuru
Vipi nchi ingakuwa, taifa bila ndururu
Taifa halingakuwa, bilashi bila ushuru

Hivi taifa kumea , nakuendelea mbele
Kwamba lajitegemea, haliwategei wale
Yataka kujitolea, ushuru bila kelele
Taifa halingakuwa, bilashi bila ushuru

Wafanyikazi wa umma, mfano mwema walimu
Wauguzi mahashuma, daktari wahadimu
Bila hizi darahima, vipi wangalihudumu?
Taifa halingakuwa, bilashi bila ushuru

Si vyema kuombaomba, kwa wageni kila mara
Huwa twajifunga Kamba, na kujitia izara
Adha zinapotukumba, kujitegemea bora
Taifa halingakuwa,bilashi bila ushuru

Miradi ya maendeleo, yahitaji darahima
Ndo tufikie upeo, ulio dunia nzima
Wadogo na wenye vyeo, bila kodi tutakwama
Taifa halingakuwa, bilashi bila ushuru

Ushuru si kwa wanyonge, wasokuwa na uwezo
Watozwe hata wabunge, na wengine wenye nazo
Yeyote asijitenge, kodi akalipa bezo
Taifa halingakuwa, bilashi bila ushuru

Kwetu kutoa ushuru,ndiko kujitegemea
Pasiwepo na udhuru, usio wa kuelea
Huwa ni kama kiguru, asenao kutembea
Taifa halingakuwa, bilashi bila ushuru

**Maswali**

a) Tambua hadhira inayolengwa katika shairi hili. (alama 1)
b) Huku ukitoa mfano,onyesha mbinu **tatu** ambazo mshairi ametumia kutosheleza uhuru wake. (alama 3)
c) Bainisha aina **tatu** za urudiaji zinazojitokeza katika utungo huu. (alama 3)
d) Eleza muundo wa ubeti wa sita. (alama 4)
e) Andika ubeti wa **nne** katika lugha ya nathari/tutumbi (alama 4)
f) Kwa kutolea mfano,taja mbinu **tatu** za kimtindo zilizotumika katika shairi hili. (alama 3)
g) Weka shairi hili katika bahari yake ukirejelea : (alama 2)
   i) Vipande

ii) Vina

**7. Soma shairi lifuatalo kisha ujibu maswali**

Sikilizeni wimbo huu:
Niliokuwa mtoto nilitwa chacha Kwa matamshi
yangu ya sasa
Nilipokuwa mtu mzima niliitwa Manywele Nilipokuwa
mwalimu nikaitwa Bure.

Huu utakuwa wimbo wako Utakapostaafu urudipo
nyumbani Umelewa kangara na nyayo zako
Zikishindwa kulenga njia nyembamba vijijini. Utakuwa
kichekesho cha watoto Watakaoukuita, Ticha! Popote upitapo.

Kumbuka mwalimu utakapostaafu, Mijusi watataga mayai
ndani ya viatu Vyako vilivyokwisha visiginino.
Na ndani ya sidiria chakavu Zilizoshikizwa
Kamba kwa pini
Mende watazaliana ndani ya chupa tupu Za marashi na za
bia.

Na manyigu yatajenga ndani ya kofia Zilizosahaulika kutani
Utakapokufa nge watazaliana Chini ya jiwe juu
ya kaburi lako, Na mlevi fulani akipita atapenga
Na kupangusa vidole kwenye jiwe pweke
Mwanzo na mwisho wako ndio huo.

Lakini wakati ungali hai
Unaweza kubadilisha mkondo wa maji Lakini kwanza
mzungumze. Wewe na mimi. Acha mioyo yote izungumzwe
Baada ya kunyanyaswa Na kisha nusu
mshahara.

Utafundisha tena nyimbo kuwasifu viongozi? Utafundisha tena
ngonjera?
Utapeleka tena wanafunzi asubuhi Wakajipange
barabarani kusubiri Mgeni afikaye saa kumi na apitapo
Apunga tu mkono kuwatia kichaa cha shangwe
Na huku nyuma mwasambaa na njaa?
Tazama hilo runda madaftari mezani Utalimaliza kwa
mshahara mkia wa mbuzi? Tuzungumze. Ninyi na mimi.
Acha mioyo yetu izungumze
Mkiwa waoga na kujikunja kama jongoo Mtawekwa
kwenye vijiti na kutupwa Nje ya ua, ndani mtawaacha
Wacheza ngoma wakitunga nyimbo mpya

Sikilizeni walimu,
Anzeni kufundisha hesabu mpya
Mjinga mmoja kujumlisha na wezi ishirini Ni sawa na sifuri.
Hapana utawala Fundisheni historia historia mpya
Hapo zamani za sasa Hapakuwa na
serikali.

Sikilizeni kwa makini Umoja hatuna
Twasambaratika kama nyumba Tulicho nacho
ni woga,
Na kinachotuangusha ni unafiki. Lakini tusikate tamaa
kama mbuni. Tukiupata umoja bado tunayo silaha.
Kura.

**Maswali**

***a)*** Fafanua sifa za shairi huru zinazojitokeza katika shairi hili. (al. 5)

***b)*** Eleza jinsi maudhui ya utamaushi yanavyojitokeza ukimrejelea nafsi-nenewa. (al. 4)

***c)*** Nafsi-nenewa anapaswa kujilaumu kwa masaibu yake. Thibitisha. (al. 2)

***d)*** Bainisha nafsi-neni katika shairi hili. (al. 1)

***e)*** Taja toni ya shairi hili. Toa mfano. (al. 2)

*f)* Eleza matumizi mawili mawili ya usambamba na jazanda katika shiri hili. (al. 4)

*g)* Eleza maana ya kufungu kifuatacho:

Mjinga mmoja kujumlisha na wezi ishirini ni sawa na sufuri. (al. 2)

## SEHEMU E: FASIHI SIMULIZI

**8. Soma utungo ufuatao kisha ujibu maswali**

**1.** Angole angole mwanangu
Mwanangu nakuchombeza
Nakuchombeza ulale
Ulale ukiamka
Nikupikie ubwabwa
Na mchuzi wa papa
Ukilia waniliza, wanikumbusha
Ukiwa wa baba na mama

**2.** Baba na mama watende
Ilimu kunikatizia
Ng'ombe, mbuzi kupokea
Kunioza dumu kongwe
Haliuki na halende
Kazi kupiga matonge

**3.** Likingia mvunguni
Lavunjavunja vikombe
Likilala kitandani
Languruma kama gombe

a) Bainisha kipera cha utungo huu. Thibitisha. (alama 2)

b) Eleza ujumbe unaofumbwa katika wimbo huu. (alama 5)

c) Tambua mbinu za kifani ambazo zimetumiwa kuwasilisha utungo huu. (alama 3)

d) Bainisha shughuli mojamoja ya kijamii na ya kiuchumi ambazo huendelezwa katika jamii ya utungo huu. (alama 2)

e) Unakusudia kukusanya data kuhusu kipera hiki. Eleza manufaa manne ya kutumia mahojiano. (alama 4)

f) Kipera hiki kinazidi kufifia katika jamii yako. Fafanua njia nne ambazo jamii ya kisasa inaweza kutumia kukuza na kuendeleza kipera hiki. (alama 4)

# GOLDLITE ONLINE SUPPLIES

***Hati ya kuhitimu kisomo cha sekondari kenya(kcse)***

# MITIHANI YA PAMOJA YA SHULE ZA KITAIFA 2025

**Jina**:……………………………………………………..……….**Nambari**:………………..…………

**Sahihi ya Mtahiniwa:**……………………….. **Tarehe:**…………..…………..**2025**

# MTIHANI WA PAMOJA WA MIRROR

**102/3**

**KISWAHILI**

**KARATASI YA PILI**

**Maagizo**

*a)* Jibu maswali manne pekee.
*b)* Swali la kwanza ni la lazima.
*c)* Maswali hayo mengine matatu yachaguliwe kutoka sehemu nne zilizobaki yaani: Riwaya, Ushairi, Hadithi fupi na fasihi simulizi.
*d)* Usijibu maswali mawili kutoka sehemu moja.
*e)* Majibu yote lazima yaandikwe kwa lugha ya Kiswahili.
*f)* Majibu yote sharti yaandikwe kwenye kijitabu cha majibu ulichopewa.
*g)* Karatasi hii ina kurasa 15 zilizopigwa chapa.
*h)* Watahiniwa ni lazima wahakikishe kwamba kurasa zote za karatasi hii zimepigwa chapa sawasawa na kuwa maswali yote yamo.
***i)*** Andika nambari ya maswali uliyoyajibu kwenye jedwali ulilochorewa hapo chini.

**Kwa matumizi ya mtahini pekee**

| Swali | Upeo | Alama |
|---|---|---|
| | 20 | |
| | 20 | |
| | 20 | |
| | 20 | |
| Jumla | 80 | |

## SWALI LA LAZIMA
## SEHEMU YA A: USHAIRI

**1. Soma shairi lifuatalo kisha ujibu maswali yanayofuata.**

Amka amsha mwili,ukanyage ardhini
Amka pia akili,usingie mashakani
Amka kiwiliwili,usingizi ulaani
Amka fanya shughuli,nchi ipo hatarini

Amka wewe jasiri,hivi unalala nini?
Amka sio kuzuri,umetegemea nini?
Amka kuna dosari ,mchanga kitumbuani
Amka fanya shughuli,nchi ipo hatarini

Amka wewe jen Zi,amsha pia jirani
Amka kipya kizazi ,usikubali uhuni
Amka ufanye kazi,mkono wende kinywani
Amka fanya shughuli, nchi iko hatarini.
**(Chotara Mswahili)**

**Maswali**

**a)**Liweke shairi hili katika bahari tatu huku ukidhibitisha. (alama 3)
b)Eleza dhamira ya mshairi. (alama 3)
c)Eleza muundo wa shairi hili. (alama 4)
d)Eleza mbinu ambazo mshairi ametumia kukidhi mahitaji ya kiarudhi. (alama 3)
e)Tambua mbinu tatu za lugha alizotumia mshairi. (alama 3)
f)andika ubeti wa pili kwa lugha ya nathari. (alama4)

## SEHEMU YA B: Tamhilia –Timothy M Arege:Bembea ya Maisha
### Jibu swali la 2au la 3

**2. Soma dondoo lifuatalo kisha ujibu maswali yanayofuata:**

...lakini ndio tabia yenu wanawake.Miaka inaposonga kama hivi mnatuona kama... kama... kama... kama vile tambara bovu.

a)Eleza muktadha wa dondoo hili. (alama 4)
b) Eleza umuhimu wa msemaji katika kukuza ploti. (alama 4)
c)Tambua mbinu nne za kimtindo katika dondoo hili. (alama 4)
d)Kwa kutoa hoja nane kutoka kwa Tamthilia eleza ni vipi utamaduni ulivyothaminiwa katika jamii hii ya Bembea ya Maisha. (alama 8)

**AU**

3.Jadili nafasi ya mwanamke katika jamii ya Bembea ya Maisha. (alama 20)

## SHEMU YA C:Riwaya ya Nguu za Jadi-Prof Clara Momanyi
### Jibu swali la 4 au la 5

**4.Soma dondoo kisha ujibu maswali yanayofuta ;**

*Watategemewa na nani maishani? Hiki ndicho kizazi cha kesho au kizazi kilichopotea tayari?*

a)Weka dondoo hili katika muktadha wake. (alama 4)
b)Tambua toni katika mazungumzo haya. (alama 2)
c)Onyesha ni vipi kizazi cha leo na cha kesho kilivyopotea. (alama 12)

**AU**

**5.**Fafanua ufaafu wa anwani ya ,'Nguu za Jadi'. (alama 20)

**SEHEMU YA D: Diwani ya Mapambazuko ya Machweo na Hadithi zingine.**

**Jibu swali la 6 au la 7**

**6.Soma dondoo kisha ujibu maswali yanayofuata.**

*Akainama chini kwenye tendeguu moja la kitanda cha besera.Akachukua kibatari cha kiberiti ili awashe taa.Mimi,nikiwa mle mvunguni.sasa kwa hakika nilishamjua shetani wa mzimu ule ni nani.Kumbe hakuwa shetani wala Kipwerere*!

a)Yaweke maneno haya katika muktadha wake. (alama 4)

b)Fafanua mbinu za kimtindo katika dondoo hili. (alama 4)

c)Onyesha umuhimu wa mandhari katika dondoo hili. (alama 4)

d)Wanakijiji waliuogopa mzimu wa Kipwerere kiasi cha kuuabudu na kutoufanyia mzaha. Thibitisha kauli hii. (alama 8)

**AU**

**7.** Kimyakimya analikariri;

*Mteule nimechoka ,kila siku kusikiya,*
*Vyereje nchi hakika,visanga kupindukiya,*
*Tunazidi filisika ,**walaji kujijaziya***
*Msiba kujitakia, kweli hauna kiliyo.*

a)Huu ni ubeti wa shairi katika hadithi"Msiba wa Kujitakia'.Eleza sababu ya mwandishi kutumia mbinu hii katika usimulizi. (alama 6)

b)Thibitisha ukweli wa kauli iliyopigiwa mstari katika dondoo. (alama 8)

c)Bainisha maudhui mbalimbali yanayojitokeza katika kifungu hiki. (alama 6)

**SEHEMU YA E :FASIHI SIMULIZI**

**8)**. (a) Huku ukitoa mifano, eleza maana ya vitanza ndimi. (alama 2)

(b) Fafanua majukumu sita ya vitanza ndimi katika jamii. (alama 6)

(c) Eleza mbinu sita utakazotumia katika kukusanya na kuhifadhi habari kuhusu vitanza ndimi. (alama 12)

# GOLDLITE ONLINE SUPPLIES

*Cheti cha Kuhitimu Kisomo cha Sekondari*

**TATHMINI YA MAJARIBIO (I), 2025**

**102/3 Kiswahili - Fasihi Karatasi ya 3**

**Saa: 2½**

# MTIHANI WA PAMOJA WA MOKASA I

***Jina: …………………………………………... Nambari ya Mtahiniwa: ……………………***

***Sahihi ya Mtahiniwa: ……………………… Tarehe: ………………… Mkondo: …………….***

***Maagizo***

a) *Andika jina lako na nambari yako ya mtihani katika nafasi ulizoachiwa hapo juu.*
b) *Tia sahihi yako kisha uandike tarehe ya mtihani katika nafasi ulizoachiwa hapo juu.*
c) *Jibu maswali* ***manne*** *pekee.*
d) *Swali la* ***kwanza*** *ni la* ***lazima****.*
e) *Maswali hayo mengine* ***matatu*** *yachaguliwe kutoka sehemu* ***nne*** *zilizobaki; yaani:* ***Tamthilia, Riwaya, Ushairi*** *na* ***Hadithi Fupi****.*
f) *Usijibu maswali* ***mawili*** *kutoka* ***sehemu moja****.*
g) *Majibu yote* ***lazima*** *yaandikwe kwa lugha ya Kiswahili.*
h) *Majibu yote* ***sharti*** *yaandikwe kwenye kijitabu cha maswali.*
i) ***Karatasi hii ina kurasa 6 zilizopigwa chapa.***
j) ***Watahiniwa ni lazima wahakikishe kwamba kurasa zote za karatasi hii zimepigwa chapa sawasawa na kuwa maswali yote yamo.***

***Kwa Matumizi ya Mtahini Pekee***

| ***Swali*** | ***Upeo*** | ***Alama*** |
|---|---|---|
| ***1.*** | ***20*** | |
| | ***20*** | |
| | ***20*** | |
| | ***20*** | |

## SEHEMU YA A: FASIHI SIMULIZI

### 1. LAZIMA

***Soma makala yafuatayo kisha ujibu maswali*.**

(*Wazee wanne wa umri wa makamo wameketi kuunda mduara. Katikati ya mduara huo, kuna babu aliyempakata mtoto mdogo. Mtoto aliyepakatwa ni mdogo na ambaye hajafika umri wa kuzungumza. Babu ameshika ugoro mkononi*)

**Babu**: (Kwa mtoto) Unaitwa nani? (Mtoto ananyamaza tu. Anaonekana kutoelewa yanayofanyika katika mazingira yake) Unaitwa nani? Je, Wewe ni Kipkech?

**Wazee**: (Kwa pamoja) Huyu siye Kipkech. Amekataa kabisa.

**Babu**: (Akimpaka mtoto ugoro puani.) Unaitwa nani? Tuambie jina lako. Wazee wamechelewa kupeleka mifugo malishoni. Unaitwa Kipsimam? ... Maritim? Je, unaitwa Nusu?

**Mzee I:** Ni kama huyu mzee amejificha. Ama alikuwa mwoga alipokuwa hai? Ama amekasirika? Mwongezee ugoro. Huenda anataka zawadi ili ajitambulishe.

**Babu**: (Akimpaka mtoto ugoro puani.) Je, Unaitwa Chepkiyeng? (Mtoto anaenda chafya) Oyee! Karibu Chepkiyeng. Karibu nduguye Nusu. Karibu mzee wetu wa bidii.

**Wazee**: (Wakishangilia) Karibu Chepkiyeng. Mzee mwanzilishi wa maduka tunayotumia hadi sasa. Karibu babu yetu! (Wote wanaanza kunywa buzaa iliyo mtungini kwa mrija huku wakizungumza kwa furaha.)

**Maswali**

(a) Ainisha kipera hiki cha fasihi simulizi. (alama 2)

(b) Bainisha sifa za utanzu ambapo kipera hiki kimetolewa. (alama 4)

(c) Umepewa nafasi ya kuwasilisha utanzu huu mbele ya hadhira. Eleza sifa **nne** unazofaa kuwa nazo. (alama 4)

(d) Bainisha shughuli **mbili** za kiuchumi katika jamii inayorejelewa katika kifungu hiki. (alama 2)

(e) Umeamua kutumia kalamu na karatasi (maandishi) kukusanya na kuhifadhi data ya fasihi simulizi. Eleza udhaifu wa mbinu hiyo. (alama 4)

(f) Fafanua changamoto **nne** zinazoweza kukukabili nyanjani, unapoenda kukusanya data kuhusu kipera hiki. (alama 4)

## *SEHEMU YA B:* TAMTHILIA

**T.M. Arege:** *Bembea ya Maisha*

*CONTACT US ON:*
*WhatsApp/Call or Text 0724351706/0726960003*
*EMAIL: Goldlitepublishers@gmail.com*

*Jibu swali la 2 au 3*

2. "Japo nilipungukiwa na mengi niliyoyatamani, nilitaka nyinyi muote mbawa mpae juu angani na kuitazama dunia kutoka kule juu kwa niaba yangu."

a) Eleza muktadha wa dondoo hili. (alama 4)
b) Bainisha aina **mbili** za taswira zinazojitokeza kwenye dondoo. (alama 4)
c) Onyesha toni inayopatikana kwenye dondoo hili. (alama 2)
d) Eleza umuhimu wa mandhari ya dondoo hili. (alama 4)
e) Fafanua sifa za msemewa katika dondoo hili. (alama 6)

3. a) Onyesha jinsi mwandishi alivyotumia mbinu ya kinaya kujenga hadithi ya **Bembea ya Maisha**. (alama 10)

b) **Bembea ya Maisha** ni tamthilia ya mabadiliko. Thibitisha. (Alama 10)

## SEHEMU YA C: RIWAYA

### C. Momanyi: *Nguu za Jadi*

*Jibu swali la 4 au la 5*

4. Kamwe hangekubali kuwa mtu wa kuomba omba misaada na ufadhili kutoka kwa wale walio navyo. Aliumbwa mkamilifu, akili timamu na siha mwilini. Kwa nini basi aombe wale waliokirimiwa vitu kama yeye? Ni ada ya binadamu kufanya kazi ili aweze kulisukuma gurudumu la maisha.

a) Eleza muktadha wa dondoo hili. (alama 4)
b) Bainisha toni katika dondoo hili. (alama 2)
c) Fafanua maudhui katika dondoo hili. (alama 3)
d) Eleza sifa **tatu** za anayerejelewa kwa kurejelea riwaya ya **Nguu za Jadi**. (alama 8)
e) Fafanua jinsi wahusika mbalimbali kwenye riwaya ya **Nguu za Jadi** wanavyofanikisha kauli iliyopigiwa mstari. (alama 8)

5. (a) Changanua mtindo katika dondoo lifuatalo. (alama 6)

Kuna waliookota chupa za plastiki kwenda kuchuuza. Kuna waliobobea katika kuchakura taka ili kupata mikebe iliyotupwa. Kisha waliichuuza mjini. Ukifika majaani,kitu cha kwanza kinachokukaribisha ni harufu kali ya uvundo uliosambaa kila mahali. Kila dakika magari yaliyosaki taka kutoka katika mitaa ya mji yalifika hapa kutupa taka. Mafalahi waliochoka na maisha waliishi mahali hapa. Walisitiriwa na makombo ya vyakula kutoka katika jaa hili kuu. Walinyanganyana chakula na kunguru waliojaa mahali hapa.

b) Bainisha toni inayojitokeza katika dondoo hili. (Alama 2)
c) Jadili mbinu walizotumia raia wa Matuo kujikomboa kutokana na uongozi dhalimu wa Mtemi Lesulia. (Alama12)

## SEHEMU YA D: USHAIRI

*Jibu swali la 6 au 7*

**5. Soma shairi hili kisha ujibu maswali.**

Pindi ilipomjia, habari za binti kazaliwa

Uso ulimsawijika, kwa soni akachanganyikiwa

"Hii ni nakhusi?

Aka, na nakama!

La, ni neema!

Bali si beluwa?"

Wapi uso aufiche?

Au mchangani auzike?

Izara hii asiipate!

Ya kuzaliwa mke.

Nitawatolea kisa…

Nawatangulizia sasa,

Kisa kilichoanza.,

Hakijawahi kukoma,

Kote kimeenea,

Namna wanavvomtesa,

Kiumbe dhalili wamemfanya,

Lini atathaminiwa?

Kisa chenyewe kitendawili,

Mwenyewe busara atoe tawili,

Ya haya mambo mawili,

Maisha bila mke ni awali,

Kisa kingeendelea?

Lulu iliyohifadhiwa ni ya pili,

Kisa kingeendelea?

**MASWALI**

a) Thibitisha kuwa shairi hili ni huru. (alama 3)
b) Eleza maudhui yanayojitokeza katika shairi hili. (alama 2)
c) Andika ubeti wa **tatu** katika lugha nathari. (alama 4)
d) Tambua matumizi ya mishata katika shairi hili. (alama 2)
e) Taja na ueleze mbinu za lugha zilizotumika. (alama 2)
f) Eleza umuhimu wa mke katika shairi. (alama 2)
g) Eleza jinsi mtunzi alivyotumia uhuru wake. (alama 2)

h) Eleza jinsi maneno haya yalivyotumika katika shairi. (alama 3)

i. Nakama
ii. Awali
iii. izara

**6. Soma shairi lifuatalo kisha ujibu maswali.**

Lau kama ingakuwa, madhali tuna uhuru,
Watu kodi kutotowa, na kuifanya kufuru,
Vije nchi ingakuwa, taifa bila kufuru,
Taifa halingakuwa, bilashi bila ushuru.

Hivi taifa kumea, na kuendelea mbele,
Kwamba lajitegemea, haliwatege'i wale,
Yataka kujitolea, ushuru bila kelele,
Taifa halingakuwa, bilashi bila ushuru.

Wafanyikazi wa umma, mfano mwema walimu,
Wauguzi mahashuma, daktari wahadimu,
Bila hizi darahima, vipi wangalihudumu?
Taifa halingakuwa, bilashi bila ushuru.

Si vyema kuombaomba, kwa wageni kila mara,
Huwa twajifunga kamba, na kujitia izara,
Adha zinazotukumba, kujitegemea bora,
Taifa halingakuwa, bilashi bila ushuru.

Miradi ya maendeleo, yahitaji darahima,
Ndo tufikie upeo, ulio dunia nzima,
Wadogo na wenye vyeo, bila kodi tutakwama,
Taifa halingakuwa, bilashi bila ushuru.

Ushuru si kwa wanyonge, wasokuwa na uwezo,
Watozwe hata wabunge, na wengine wenye nazo,
Yeyote asijitenge, kodi akalipa bezo,
Taifa halingakuwa, bilashi bila ushuru.

Kwetu kutoa ushuru, ndiko kujitegemea,
Pasiwepo na udhuru, usio wa kuelea,
Huwa ni kama kiguru, asenao kutembea,
Taifa halingakuwa, bilashi bila ushuru.

**(Joseph Kiponda)**

Maswali:

a) Chambua maudhui katika shairi hili. (alama 4)
b) Eleza muundo wa shairi hili. (alama 4)
c) Bainisha aina **tatu** za urudiaji katika shairi hili. (alama 3)

d) Bainisha bahari zinazojitokeza katika shairi hili kwa kuzingatia vigezo vifuatavyo:(alama 2)
   i. Mpangilio wa vina
   ii. Idadi ya vipande katika kila mshororo
e) Fafanua aina **tatu** za uhuru wa kishairi katika shairi hili. (alama 3)
f) Andika ubeti wa **sita** kwa lugha nathari. (alama 4)

## SEHEMU YA E: HADITHI FUPI

**Clara Momanyi:** *Mapambazuko ya Machweo*

8. Utumwa mamboleo ndio huu. ***Ubedui uliogubikwa ndani ya ukawaida wa maisha*** ya kisasa ndio huu.

a) Eleza muktadha wa dondoo hili. (alama 4)
b) Huku ukitoa mifano kutoka hadithi zifuatazo, thibitisha kuwa: **'Ubedui umegubikwa ndani ya ukawaida wa maisha.'**
   (i) Mapambazuko ya Machweo (alama 5)
   (ii) Msiba wa Kujitakia (alama 5)

**W. N. Ogenche:** ***Sabina***

(c) "*Samahani mwalimu, nina majukumu mengi ya kutekeleza nyumbani kabla ya kuja shuleni kila asubuhi*." Eleza jinsi msemaji alivyotumika kuwakuza wahusika wengine hadithini. (alama 6)

# GOLDLITE ONLINE SUPPLIES

*Hati ya kuhitimu kisomo cha sekondari kenya(kcse)*

# MITIHANI YA PAMOJA YA SHULE ZA KITAIFA 2025

**Jina:………………………………………………………..……….Nambari:…………………..…………**

**Sahihi ya Mtahiniwa:……………………….. Tarehe:………….…………..2025**

# MTIHANI WA PAMOJA WA MOMALICHE

**102/3**

**KISWAHILI**

**KARATASI YA PILI**

**Maagizo**

*a)* Jibu maswali manne pekee.
*b)* Swali la kwanza ni la lazima.
*c)* Maswali hayo mengine matatu yachaguliwe kutoka sehemu nne zilizobaki yaani: Riwaya, Ushairi, Hadithi fupi na fasihi simulizi.
*d)* Usijibu maswali mawili kutoka sehemu moja.
*e)* Majibu yote lazima yaandikwe kwa lugha ya Kiswahili.
*f)* Majibu yote sharti yaandikwe kwenye kijitabu cha majibu ulichopewa.
*g)* Karatasi hii ina kurasa 15 zilizopigwa chapa.
*h)* Watahiniwa ni lazima wahakikishe kwamba kurasa zote za karatasi hii zimepigwa chapa sawasawa na kuwa maswali yote yamo.
***i)*** Andika nambari ya maswali uliyoyajibu kwenye jedwali ulilochorewa hapo chini.

**Kwa matumizi ya mtahini pekee**

| Swali | Upeo | Alama |
|---|---|---|
| | 20 | |
| | 20 | |
| | 20 | |
| | 20 | |
| Jumla | 80 | |

**CONTACT US ON:**
**WhatsApp/Call or Text 0724351706/0726960003**
**EMAIL: Goldlitepublishers@gmail.com**

## SEHEMU YA A: FASIHI SIMULIZI

**1.** Soma utungo ufuatao kisha ujibu maswali yanayofuata.

Hapo zamani za kale paliishi sungura na ndovu. Wanyama hawa waliishi baharini.Maulana alikuwa amewatunukia mapenzi si haba.Makazi yao yalikuwa yamepambwa yakapambika.Walitegemea matunda mbalimbali yaliyokuwa baharini kama mapera, matomoko matikitimaji na kadhalika.

Siku moja usiku wa manane, maji yakaanza kupwa.Ndovu aliathirika zaidi. Alijaribu kuinama majini lakini hakuweza . Alimwita sungura amsaidie lakini sungura alikuwa ametoweka. Ndovu aliamua kwenda kumtafuta sungura. Alimtafuta hadi msituni lakini hakumpata. Alihofia kurudi baharini na hadi wa leo yumo msituni.

Maswali

a) Tambua utanzu na kipera chake. (alama2)

b) Taja fomyula zingine mbili za kutanguliza kifungu hiki. (alama2)

c) Eleza umuhimu wa kijipera hiki. (alama5)

d) Eleza sifa za kifungu hiki. (alama5)

e) Eleza umuhimu wa fomyula:

**(i)** Kutanguliza (alama3)

**(ii)** Kuhitimisha (alama3)

## SEHEMU YA B: TAMTHILIA

### T.M. Arege: Bembea ya Maisha"

*Jibu swali la 2 au la 3*

**2.** Soma dondoo lifuatalo kisha ujibu maswali yafuatayo:

"Nikimaliza kesho tutaenda out?"

(a) Eleza muktadha wa dondoo (alama4)

(b) Jadili jinsi msemaji wa maneno haya:

*(i)* Anavyochangia katika kukuza migogoro katika tamthilia (alama3)

*(ii)* Anavyojenga msemewa katika dondoo hili (alama3)

(c) Thamani ya mtoto wa kike imepanda na nafasi yake kupanuka. Thibitisha hili ukirejelea tamthilia "Bembea ya maisha" (alama10)

**3.** (a) "Ninaweza kuiachia dunia tabasamu", mnenaji ametimizaje kauli hii. (alama10

(b) Mabadiliko yamesheheni katika Tamthilia ya Bembea.Thibitisha. (alama10

## SEHEMU YA C: USHAIRI

*Jibu swali la 4 au la 5*

**4.** Soma shairi lifuatalo kisha ujibu maswali.

MAZINGIRA

Chochote tulojaliwa, lichopewa na manani,
Linapoangaza juwa, kinapendeza machoni,
Tangu jadi lilijuwa, huepuka asilani,
Ndicho bora nakwambiya, tega sikio sikia.

Mwanzoni ni kujijua, ni wapi unaselea,
Endapo ipo mvua, kipupwe au ni jua,
Yapaswa kuzingatia, hali anga angalia,
Akili ukiitia, mambo haya murua.

Usafi wa mazingira, utaanzia mwilini,
Nacho chumba kiwe bora, angaza macho pembeni
Sikione cha kukera, hakikisha mebaini,
Panga chumba kipangike, mpango wa kuvutia.

Asubuhi kiamka, utakoga sikatai,
Baadaye utataka, nadhifu uwe hai,
Osha bafu ukitoka, nacho choo ninadai,
Hivi vyote ni muhimu, siku zote zingatia.

Uvumapo 'pepo' kali, ni majani hudondoka,
Tizama kila mahali, kufagia lodondoka,
Uchafu wa kila hali, ondoa pasi kuchoka,
Mazingira tapendeza, ukitaka yapendeze.

La msingi kuepuka, utupaji taka ovyo,
Pande zote tachafuka, mazingira kuwa ovyo,
Uokote takataka, latapakaa kiovyo,
Uwe na shimo la taka, kweka visivyofaa

Nifikapo ukingoni, raha hino natambua,
Usafi kuzingateni, mazingira tavutia,
Hima basi naimbeni? Suala hili fikiria,
Tuyaepuke maradhi, kwa kutunza maringira

Maswali

(a) Shairi hili ni la aina gani? (alama2)
(b) Shairi hili ni la bahari gani? (alama3)
(c) Eleza njia mbili za kuhifadhi mazingira kulingana na mtunzi (alama2)
(d) Kwa kutoa mifano kutokana na shairi hili, eleza mbinu za lugha katika shairi hili (alama4)
(e) Kichwa cha shairi hili kinaoanaje na maudhui ya shairi (alama2)
(f) Andika ubeti wan ne kwa lugha nathari (alama4)
(g) Eleza mbinu alizotumia mshairi kutosheleza mahitaji ya kiarudhi (alama3)

**5.** Soma shairi lifuatalo kisha ujibu maswali.

SIWATI

Siwati nshishiyelo, siwati; kwani niwate?
Siwati ni hilo , 'talishika kwa vyovyote
Siwati ni mimi nalo, hapano au popote
Hadi karibuni sote, mimi nalo tufukiwe

**CONTACT US ON:**
**WhatsApp/Call or Text 0724351706/0726960003**
**EMAIL: Goldlitepublishers@gmail.com**

Siwati ngaadhibiwa, adhabu kila mfano
Siwati ningaambiwa, 'tapawa kila kimono
Siwati lililo sawa, silibanduwi mkono
Hata ningaumwa meno, mkono siubanuwi

Siwati si ushindani, mukasema nashindana
Siwati ifahamuni , sababuye waungwana,
Siwati ndangu imani, niithaminiyo sana
Na kuiwata naona, itakuwa ni muhali

Siwati nimeradhiwa, kufikwa na kila mawi
Siwati ningaambiwa, niaminiyo hayawi
Siwati kasha nikawa, kama nzi ; hivyo siwi
Thamma nakariri siwi, na Mn'gu nisaidiya
*(Kutoka sauti ya Dhiki; Abdlitif Abdalla)*

Maswali:

(a) Thibitisha kuwa shairi hili ni la arudhi (alama5)
(b) Malenga ana maana gani anaposema:
   (i) Siwati ningaambiwa, 'tapawa kila kimono (alama3)
   (ii) Siwati nimeradhiwa, kufikwa na kila mawi (alama3)
(c) Eleza mshororo wa mwisho katika kila ubeti wa shairi hili (alama3)
(d) Shairi hili li katika bahari gani? (alama4)
(e) Mwandishi ametumia mbinu gani katika maneno 'talishika,' 'mukasema' (alama2)

## SEHEMU D: HADITHI FUPI

**D.W Lutomia na Phibbian Muthama: Mapambazuko ya Machweo na Hadithi Nyingine**

*Jibu swali la 6 au la 7*

**6.**

R. Wangari: "Fadhila za Punda"

(a) Soma dondoo lifuatalo kisha ujibu maswali yafuatayo:

Ni kama urafiki wa paka na panya, siku moja panya huenda akawa kitoweo kuridhisha matilaba yake paka. Si hali ya kumpa utulivu … hasa ikitiliwa maanani kuwa panya mwenyewe … Anayemlinda kama mboni ya jicho lake. Afanye nini…?

Maswali

a) Eleza muktadha wa dondoo hili (alama4)
b) Tambua toni ambayo imetumika katika dondoo hili (alama1)
c) Jadili jinsi urafiki unaorejelewa umekuwa wa paka na panya (alama5)

**C. Momanyi: "Mapambazuko ya Machweo"**

(b) Soma dondoo lifuatalo kisha ujibu maswali yafuatayo:

"Nilidhani wewe ni Rafiki wa dhati kumbe hasidi mkubwa…"

a) Eleza muktadha wa dondoo (alama4)
b) Fafanua sifa mbili za msemaji katika dondoo hili (alama2)
c) Kwa kurejelea hadithi ya "Mapambazuko ya Machweo" Jadili suala la unafiki (alama4)

**CONTACT US ON:**
**WhatsApp/Call or Text 0724351706/0726960003**
**EMAIL: Goldlitepublishers@gmail.com**

**7.**

**D.W. Lutomia: "Msiba wa Kujitakia"**

(a) Soma dondoo lifuatalo kisha ujibu maswali yafuatayo:

"Tuwe watulivu jamani, subira huvuta heri. Mgeni wetu…. Atafika wakati wowote kuanzia sasa. Subira… subira… subira ndugu zangu."

Maswali

a) Eleza muktadha wa dondoo hili (alama4)
b) Tambua mbinu mbili za kimtindo katika dondoo hili (alama2)
c) Eleza sifa za mgeni anayetarajiwa kwa mujibu wa dondoo hili (alama4)

**P. N. Mutua: "Harubu ya Maisha"**

(b) Soma dondoo lifuatalo kisha ujibu maswali yafuatayo:

"Enhee! Mpaka sasa hukupata nafasi ya kupiga simu, au aghalau kutuma arafa?"
"Samahani … ulipopiga nilikuwa barabarani singeweza kupokea simu."

a) Eleza muktadha wa dondoo hili (alama4)
b) Eleza vipengele viwili vya kimtindo katika dondoo hili (alama2)
c) Harubu ni sehemu ya maisha ya binadamu. Hakiki kauli hii kwa kurejelea hadithi "Harubu ya Maisha" (alama4)

**SEHEMU YA E: RIWAYA: NGUU ZA JADI**
**C. Momanyi: Nguu za Jadi**

**8.** Soma dondoo lifuatalo kisha ujibu maswali yafuatayo:

*"Mhn, ati familia? Kwani mimi mjinga niache mapesa haya yote yanipite bila kuyafaidi. Kipato ni hicho… kidogo hata hakiwezi kuilisha jamaa yangu kwa juma moja. Potelea mbali. Mangwasha na wanawe watajipanga. Pombe ya bwerere siachi ng'o! Najua Sagilu alimpenda sana Mangwasha wakati mmoja. Lakini si sasa. Hana haja naye. Kwani akina sihaba wako wapi? Aaah Mrima, vunja mifupa ukiwa bado una meno bwana."*

Maswali

**(a)** Changanua mtindo katika dondoo hili (alama6)
**(b)** Eleza maudhui yanayojitokeza katika kifungu hiki (alama4)
**(c)** Onyesha jinsi mwandishi alivyotumia mbinu ya sadfa katika uwasilishaji wake ukirejelea riwaya hii ya Nguu za jadi (alama10)

**CONTACT US ON:**
**WhatsApp/Call or Text 0724351706/0726960003**
**EMAIL: Goldlitepublishers@gmail.com**